# Nipashe

Jumatatu Mei 30, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580961

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



SportPesa

JACKPOT BABA LAO!

TZS. 233,880,320

CHEZA SASA KWA 1000/= TU!

SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#




## Mtuhumiwa ubakaji auawa na wananchi wenye hasira

UKURASA 3



## KLOPP: MSIHOFU TUTAKUWA KWENYE FAINALI IJAYO UEFA

UKURASA 21

# Hoja 25 za mabadiliko ya Sheria Vyama vya Siasa

- **ACT** yataka usajili wa vyama ufanywe na tume huru...

*Endelea ukurasa 2*



Katibu Mkuu wa ACT Wazalendo, Ado Shaibu, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana kuhusu mapendekezo yaliyowasilishwa kwenye kikosi kazi cha Rais. **PICHA: IKULU**

## Wabunge wahamaki vitendo ukatili kingono kushamiri

UKURASA 4



Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Mabenki Kenya, Julius Alengo (kushoto) akimkabidhi tuzo Mweka Hazina wa Benki ya NMB, Aziz Chacha ambaye alipokea tuzo ya Ofisa Mtendaji Mkuu Bora Afrika kwa Mwaka 2022 (Tanzania) kwa niaba ya Ruth Zaipuna ambaye hakuwepo katika hafla hiyo iliyofanyika Nairobi mwishoni mwa wiki.

## Mume akimbia akidaiwa kumuua mke kwa risasi

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store



MICHEZO FEI TOTO AANIKA UDHAIFU SIMBA UK.24

MAONI, KATUNI UK.6



Ofisa mradi wa kuwawezesha watoto wa kike uliopo chini ya Shirika la Worldvision, Neema Mwambo (mwenye kofia), akimuonyesha mgeni rasmi, Ofisa Tawala wa Wilaya ya Karatu, Jackline Rwezaura taulo za kike zilizotengenezwa na wanafunzi kwenye uwanja wa Shule ya Msingi Endabash yalipofanyika maonyesho ya Siku ya Hedhi Duniani. **PICHA: DANIEL SABUNI**

# Hoja 25 mabadiliko Sheria Vyama Siasa

## ■ACT yataka usajili wa vyama ufanywe na tume huru

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, amesema chama chake kimependekeza mabadiliko makubwa kwenye Sheria ya Vyama vya Siasa kwa lengo la kuweka uwanja huru kwa vyama vyote kutekeleza wajibu wa kisiasa bila kuingiliwa na serikali.

Amesema mapendekezo hayo yaliyowasilishwa kwenye kikosi kazi cha Rais, yameridhiwa na kamati kuu ya chama hicho kilichokutana hivi karibuni mjini Unguja na kujadili kwa kina mabadiliko yaliyofanywa mwaka 2019 kuwa yaliyofuta uhai wa vyama vya siasa na kujenga himaya ya chama chenye serikali iliyopo madarakani.

Ado alitoa kauli hiyo jana jijini Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari, akieleza kwa kina masuala waliyowasilisha kwenye kikosi kazi cha Rais.

"Mabadiliko ya Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 2019 yamefuta uwapo wa vyama vya siasa hai na kujenga himaya ya chama chenye serikali iliyopo madarakani kumiliki fikra zote za wananchi na hii ni hatari kwa Taifa," alisema.

Alitaja baadhi ya mapendekezo hayo kwenye sheria hiyo kuwa ni usajili wa vyama vya siasa ufanywe na tume huru, na mafunzo ya elimu ya uraia na kujiongezea uwezo yanayoandaliwa na vyama vya siasa yasidhibitiwe na Msajili wa Vyama vya Siasa.

Katibu Mkuu huyo alisema Ofisi ya Msajili izingatie masuala ya Muungano kwa Msajili na Naibu wake kutoka pande zote za Muungano, vifungu vya 4(5)(f) na 5A alivyodai vinalenga kudhibiti mafunzo yanayoandaliwa na vyama vya siasa vifutwe ili vyama viwe huru kutoa mafunzo, pia kinga ya msajili na maofisa wake kutoshitakiwa iondolewe.

Aliongeza kuwa mapendekezo mengine waliyowasilisha ni pamoja na masuala ya Muungano na usawa wa kijinsia yazingatiwe kwenye uteuzi wa Msajili na Naibu Msajili.

"Kifungu cha 8(7) kifanyiwe marekebisho ili kutamka bayana muda ambao Msajili atatakiwa kutoa usajili wa muda na wa kudumu, Kifungu 8E kuhusiana na vikosi vya ulinzi kibadilishwe kuviwezesha vyama kuwa na ulinzi wa kulinda viongozi na mali za chama," alisema.

Kuhusu usawa wa kijinsia, Ado alisema vyama viwekewe sharti la kuwa na angalau asilimia 30 ya viongozi wa kitaifa kuwa wanawake, huku akitaka iongezwe fasili (c) kwenye Kifungu cha 10(1)(c) kuweka sharti kwa vyombo vya habari vya serikali kutumikia vyama vyote kwa usawa huku kwenye mikutano ya hadhara wakitaka Jeshi la Polisi liwekewe muda ambao litapaswa kutoa mrejesho baada ya kupokea taarifa ya kufanyika kwa mkutano wa hadhara (ndani ya saa 12).

Akizungumzia ruzuku kwa vyama vya siasa, Ado alisema chama chao kinapendekeza mfumo ubadilishwe ili kila chama kilichokidhi sifa ya kushiriki uchaguzi, kutopata hati chafu, kuwa na uwakilishi wa mbunge, diwani au kiongozi wa serikali za mitaa na angalau asilimia 30 ya viongozi wanawake kupata ruzuku pamoja na kuanzishwa kwa baraza la kusuluhisha migogoro kwenye vyama vya siasa.

"Tumekuja na hoja 25 za kufanyia maboresho makubwa Sheria ya Vyama vya Siasa. Tunalenga kupunguza madaraka ya Msajili wa Vyama vya Siasa na kuiondolea jinai siasa. Kwa hoja hizi, itabidi Sheria ya Vyama vya Siasa iandikwe upya," alisema.

Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Doroth Semu, alisema wameangalia kwa kina nafasi ya usawa wa kijinsia na kutaka mfumo wa uchaguzi ubadilishwe kwa mshindi kuchukua nafasi zote za kiserikali.

Alisema katika mazingira hayo ya kutaka mfumo wa uchaguzi ubadilishwe, ACT - Wazalendo inataka kura ziwekwe kwenye asilimia na kila chama kiwasilishe majina ya wawakilishi katika ngazi husika zikilenga usawa wa kijinsia.

Aliongeza kuwa hatua hiyo itapunguza gharama za kufanya uchaguzi mara kwa mara pale kunapohitajika kuziba pengo la mwakilishi aliyepoteza sifa ya uwakilishi katika ngazi husika.

Ismail Jussa, Mjumbe wa Kamati Kuu ya ACT-Wazalendo, alisema dhamira ya chama hicho ni kuona utaratibu wa kupatikana Katiba Mpya unaanza sasa sambamba na mchakato wa kupata Tume Huru ya Uchaguzi.

"Tunataka tume huru iende sambamba na mchakato wa Katiba na kama Katiba itakuwa haijakamilika mpaka tunaingia kwenye uchaguzi, basi tume hiyo isimamie uchaguzi kwa kuwa itakuwa na sifa za kutoegemea upande wowote," alisema.

Alitaja sifa za kuwapata wajumbe wa tume huru kuwa ni watu wenye sifa kuomba nafasi hizo hususan mwenyekiti na makamu wake na kisha kuchujwa na vyombo huru kabla ya kukabidhiwa nafasi hizo na mchakato huo uende sambamba na kuwaajiri watumishi wa tume na kuwaondoa wakurugenzi katika usimamizi wa uchaguzi.

# Mume akimbia akituhumiwa kumuua mke kwa risasi

**Na Richard Makore,** MWANZA

MKAZI wa Buswelu, wilayani Ilemela mkoani Mwanza Swalha Salum (26), ameuawa kwa madai ya kupigwa risasi na mume wake kutokana na mgogoro wa kifamilia unaodaiwa kuhusishwa na wivu wa mapenzi.

Imedaiwa kuwa mwanamke huyo alipigwa risasi saa 2:00 usiku juzi nyumbani kwao eneo la Buswelu ikiwa ni miezi mitano tangu wawili hao kufunga ndoa.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi mkoani Mwanza, Ramadhan Ng'anzi, tukio hilo lilitokea nyumbani kwao baada ya kuwapo na mgogoro wa muda mrefu tangu wafunge ndoa yao.

Kamanda Ng'anzi alisema tukio hilo limeleta simanzi kwa familia na ndugu wengine na kwamba baada ya mauaji hayo mtuhumiwa alikimbia.

Alisema kutokana na sababu za kiupepelezi kwa sasa jina la mtuhumiwa wanalihifadhi na wanaendelea kumsaka mtuhumiwa ili afikishwe kwenye vyombo vya sheria.

Hata hivyo, Kamanda Ng'anzi alikanusha baadhi ya taarifa zilizosambaa jana katika mitandao ya kijamii kwamba mwanamke huyo aliuawa baada ya kutoka katika muziki uliokuwa ukipigwa na mwanamuziki Diamond, jijini Mwanza.

Aliongeza kuwa katika tamasha hilo la Diamond hakuna tukio lolote lililotokea pamoja na mchezo uliopigwa juzi kati ya timu ya Simba na Yanga.

Katika mchezo huo ambao ulikusanya maelfu ya mashabiki jijini hapo, Kamanda Ng'anzi alisema hakuna tukio lolote lililojitokeza.

Tukio la kifo cha mwanamke huyo jana lilisambazwa katika mitandao ya kijamii huku kukiwa na taarifa mbalimbali baadhi zikidai alipigwa risasi baada ya kurudi nyumbani akitoka muziki usiku.

Mmoja wa marafiki wa mwanamke wa marehemu, aliandika katika mitandao ya kijamii akidai kwamba rafiki yake aliwahi kupigwa na kitako cha bunduki na mume wake na kuzimia kabla ya tukio la juzi.

Alisema baada ya tukio hilo, jana aliamua kumpiga risasi na kumuua huku akiandika maneno ya kumuombea kwa Mungu apumzike kwa amani.



Meneja Rasilimali Watu wa Kampuni ya KIOO Limited, Jacob Msuya akipokea tuzo ya mwajiri bora kwa Wilaya ya Temeke kutoka kwa Katibu Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Sekta ya Viwanda na Biashara (TUICO) Taifa, Boniface Ntakatisi wakati wa hafla iliyofanyika mwishoni mwa wiki Dar es Salaam. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mtuhumiwa ubakaji auawa na watu wenye hasira

**Na Daniel Sabuni,** ARUSHA

MTUHUMIWA wa matukio ya ubakaji maarufu jijini Arusha kama Teleza, aliyekuwa akibaka wanawake na kuwaua, ameuawa na wananchi wenye hasira katika eneo la Murieti, mkoani Arusha jana.

Kamanda wa Polisi mkoani Arusha, Kamishna Msaidizi, Jastine Masejo, alithibitisha kuuawa kwa mtuhumiwa huyo.

Alisema tayari Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Mkoa wa Arusha (RCO), ametuma timu ya uchunguzi katika eneo la Murieti, kuhoji watu ili kujua kuwa ni yeye au ni mhalifu mwingine.

"Tunachunguza. Tumepokea taarifa kuwa kuna kijana mmoja wa maeneo ya Murieti, ameuawa na wananchi wenye hasira kali jana alfajiri wakati akitaka kufanya uhalifu, bado hatujafahamu ni nani na alikuwa akitaka kufanya uhalifu gani. Watu wanaweza wakasema ni Teleza, lakini ukakuta siye ni mtu mwingine, tunachunguza tutatoa taarifa kamili kupitia vyombo vya habari," alisema Kamanda Masejo.

Aliwataka wananchi mkoani Arusha kutojichukulia sheria mkononi na wanapobaini mhalifu watoe taarifa polisi ili kupata msaada wa kumkamata na kufikishwa kwenye vyombo vya dola ili sheria ichukue mkondo wake.

Taarifa zilizozagaa kwenye mitandao ya kijamii, zilieleza kuwa mtu huyo aliuawa saa 10 alfajiri jana katika eneo la Murieti, alipovamia katika nyumba ya mkazi mmoja (jina linahifadhiwa kwa lengo la kufanya uhalifu wa ubakaji wa watoto.

Majirani ambao hawakuwa tayari kutajwa majina yao kwa sababu za kiusalama, walisema walisikia makelele ya kuomba msaada kutoka kwa majirani wenzao na ndipo wakaungana nao, walipofika wakakuta ameshauawa.

"Tulipofika tulikuta watu wengi na gari la polisi, tukasaidia kumpakia ili apelekwe kwenye chumba cha kuhifadhia maiti cha Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha ya Mount Meru," alisema mkazi mmoja wa eneo la Murieti.

Mkazi mwingine alisema alisikia mayowe ya watu wengi na walipohoji wakaambiwa alifika katika nyumba ya jirani yao kwa lengo la kubaka mtoto, wakapiga kelele za kuomba msaada, akakimbilia kwenye paa la nyumba yake kujificha, wakampiga kwa silaha mbalimbali hadi mauti yakamkuta.

"Mimi simjui Teleza kwa sura, lakini wengi wanadai ni yeye. Kama ni mwenyewe itakuwa furaha sana maana ametesa familia nyingi kwa uhalifu wa ubakaji na wakati mwingine kuwakata kwa visu na kuwaua," alisema.

# Membe rasmi CCM, akabidhiwa kadi

**Na Beatrice Shayo**

ALIYEKUWA mgombea Urais katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, kupitia Chama cha ACT-Wazalendo, Bernard Membe ameeleza sababu zilizomfanya arejee CCM baada ya kuondoka na kutimkia upinzani.

Kadhalika amesimulia jinsi alivyoumia kutokana na uamuzi wa kuondolewa uanachama wa CCM, chama alichokulia huku akiahidi kufia ndani ya chama hicho.

Membe aliyewahi kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa katika Serikali ya Awamu ya Nne, alirejea rasmi CCM jana na kupokelewa na Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM, Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, katika mkutano wa hadhara wa Mbunge wa Mtama, Nape Nnauye uliofanyika katika Kata ya Chiponda, Jimbo la Mtama mkoani Lindi.

Alisema kurejea kwake kunatokana na dhamira ya kukitumikia chama hadi kufa.

Akizungumza katika mkutano huo, katika Kijiji cha Rondo, alisema Machi 30 hadi Aprili Mosi, mwaka huu aliitwa Dodoma, kwenye Mkutano wa Kamati Kuu ya Maadili na Mkutano Mkuu wa Halmashauri Kuu, alipewa nafasi na Mwenyekiti wa CCM Taifa kuzungumza na wana CCM.

"Mama yetu, Rais wetu na Mwenyekiti wetu wa CCM Taifa alinipa nafasi ya kuzungumza na wajumbe wa Kamati Kuu ya Chama Taifa. Nashukuru kwa kupewa nafasi ile na wajumbe waliridhia kwa kauli moja nirejee CCM.

"Nimerejea CCM kwa sababu kuu mbili, sababu ya kwanza nilishauriwa na viongozi wa dini zote, nilishauriwa na viongozi wa CCM ngazi ya wilaya na Mkoa, nilishauriwa na marafiki zangu wote nirejee CCM, nilishauriwa na wana CCM.

"Kutokana na ushauri wote huo sikuwa na namna nyingine zaidi ya kutii, nimekubaliana na ushauri wa wote waliosema nirudi CCM na sasa nimerudi CCM," alisema Membe wakati akitangaza kurejea tena kwenye chama.

Alisema sababu ya pili ya kurudi kwenye chama hicho inatokana na dhamira yake ya kukitumikia Chama Cha Mapinduzi hadi atakapokwenda kaburini. "Nilipoondolewa CCM nilisikitika sana, nilisononeka sana, na ninyi wananchi mlisikitika, mlisononeka.

"Sababu ambazo zilinifanya niondoke CCM haziko tena, narudi, sababu zilizoniondoa CCM haziko tena. Nimerudi, namshukuru Mwenyekiti wa CCM na wajumbe wa Kamati Kuu kunirudisha. Nimerudi kwenye chama ambacho nimezaliwa na kukulia, chama ambacho kimenisomesha.

Kwa upande wake Mbunge wa Jimbo la Mtama ambaye pia ni Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape alisema baada ya Membe kuondoka kwenye chama wananchi wengi walichukia, lakini aliwaomba wasichukie kwa kuwa aliamini kuna siku moja atarejea.

"Leo Mwenyezi Mungu ameturudishia faraja la Rondo, ameturejeshea furaha Chiponda. Mtama ni wastaarabu na hatuna shida tena, tuna imani kubwa na Membe, alinikabidhi kijiti na kuvaa viatu vyake, kulikuwa na mambo yaliyokwama huku nyuma kwa sababu za kisiasa, lakini Mama Samia amekuja ameziondoa," alisema.

Aliwataka wananchi wa Mtama kushikamana, fitina ambazo ziliingia kati zimekwisha. "Membe amenipigania katika mambo mengi, nilipotaka ubunge Ubungo baada ya kuonekana fitna zimeingia katikati Membe aliamua kuchora ramani."

**AKABIDHIWA KADI**

Akizungumza katika mkutano huo, Shaka alisema Membe amerudishwa katika chama baada ya kufuatwa kwa utaratibu ikiwemo kujadiliwa na tawi lake kisha na vikao vya juu.

Alisema Membe na wanachama wengine zaidi ya 1,670 waliovuliwa uanachama ambao wamejadiliwa katika vikao na kurejeshewa uanachama, sasa wanaweza kukabidhiwa kadi zao katika matawi yao.


**NAFASI (2) ZA KAZI**
**IDARA YA OPERATIONS.**

NAFASI:
TRANSPORT & LOGISTICS MANAGERS.

SIFA:
1. MWOMBAJI AWE NA ANGALAU DIPLOMA KWENYE FANI HIYO.
2. AWE NA UZOEFU USIOPUNGUA MIAKA 3 KWENYE FANI HIYO.

MAOMBI YATUMWE KWA BARUA PEPE:
tzopenings@gmail.com
KABLA YA TAREHE 14/06/2022.

116877802



**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**UPENDO HIRMAK KOMBA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA SIENTA yenye USAJILI NAMBA **T948DDL,** CHASSIS NAMBA : **NCP810056816,** ENGINE NAMBA : **INZB246673.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**DSM/PHQ/RB/210696/2022**

116877602



**KUPOTEA KWA CHETI**



**FLORIDA JOHN CHIWA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye **INDEX NAMBA S0815-0036** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MBINGA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2012. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA:DAR/ KIG/RB/205422**

116877502



**KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA**



**MNYANGALA JACOB DOMINIC** anatangaza kupotea kwa hati yake ya kusafiria (Passport) yenye namba **TAE236556** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam 2019 . Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu naye. POLISI TAARIFA:
**ARU/ARU/RB/207944/2022**

116877702



STAR CITY



COMMERCIAL & INDUSTRIAL
PLOTS FOR SALE IN MOROGORO
@ DAR - MBEYA HIGHWAY

CONTACT US FOR PRICE





* 1st Phase 300 Acres for Commercial & Industrial Use
* Land is along the Dar to Mbeya Highway
* Within Morogoro city
* Flat Land
* Plots ranging from 0.5 to 5.5 Acres
* Individual Titles will be given
* Accessability to SGR

CONTACT US... +255 715 415 145 +255 783 278 787 - +255 783 124 688 - sales.starcitytz@gmail.com

21686902



Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo akipanda ngazi za tanki la maji lenye uwezo wa kubeba lita laki 5 na kuhudumia wakazi 14,600 wa kijiji cha Mwakitolwa ikiwa ni sehemu ya ziara yake ya kukagua utekelezwaji wa ilani ya uchaguzi ya mwaka 2020-2025 mkoani Shinyanga jana. **PICHA: ADAM MZEE**

# Wabunge wahamaki watoto kufanyiwa ukatili kingono

**Na Romana Mallya,** DODOMA

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, amesimulia jinsi babu alivyokuwa akimfanyia mjukuu wake kitendo cha ukatili wa kingono kwa kumbaka na kumlawiti katika kipindi cha mwaka mmoja.

Kitendo hicho na vingine vya kikatili dhidi ya wanawake na watoto kiliwagusa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii na kutaka serikali na jamii kuja na njia za kukomesha vitendo hivyo ili kuwa na kizazi chenye ustawi na kisichokuwa na maumivu kutokana na ukatili.

Waziri Gwajima alisimulia hayo wakati wa semina ya wabunge iliyofanyika jijini hapa juzi, kuhusu Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA), utekelezaji wa masuala ya jinsia na uwezeshaji wanawake kupitia jukwaa la kizazi chenye usawa pamoja na Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto.

Alisema akiwa katika semina hiyo kupitia namba yake ya simu aliambiwa katika mkoa mmoja (ambao hakuutaja), kuna mtoto mwanafunzi amekuwa akibakwa na kulawitiwa na babu yake mfululizo kwa mwaka mmoja.

"Kuna mbunge amechangia hapa kuhusu masuala ya saikolojia, wanasaikolojia kuwapo mashuleni, ninajiuliza kama kitendo kinatokea wakati wote, kinamuathiri mtoto, hatafanya vizuri katika masomo, atakuwa analala tu au anakuwa na matatizo ya kiafya au msongo wa mawazo na anakwenda shule kuna matroni, lakini hawawezi kugundua," alisema.

Waziri Gwajima aliwaomba wabunge kuhamasisha jamii na kuijengea uelewa kuhusu kuwalinda watoto na makundi mengine wakiwamo wanawake ambao wanakabiliwa na ukatili wa kila aina.

Alisema wakati awamu ya kwanza ya MTAKUWWA ikikaribia ukingoni mwezi ujao, kuna mafanikio kadhaa yamepatikana, lakini jamii bado imesongwa na ukatili katika makundi mbalimbali.

Alisema wizara ya itafanya tathmini ya mpango huo ili kubaini mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji kwa kipindi cha miaka mitano na matatizo yaliyoathiri kufikiwa.

"Tathmini inatarajiwa kubainisha masuala ya kuigwa na kutoa mapendekezo ya namna bora zaidi ya kukabiliana na matatizo na upungufu uliobainika," alisema.

Pia, alisema wizara inaendelea kuratibu programu ya utekelezaji wa ahadi za nchi katika kutekeleza malengo ya Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa, ambayo ipo katika hatua ya ukamilishwaji ili iweze kuzinduliwa mwezi ujao na kuwaomba wabunge, wahamasishe wananchi wajue utekelezaji wa ahadi za nchi kuhusu kizazi chenye usawa husan eneo la haki za kiuchumi kwa wanawake.

Mbunge wa Viti Maalum CHADEMA, Hawa Mwaifunge, alisema upo ukatili mkubwa unaoendelea katika jamii, lakini sio waathirika wote wanaoweza kwenda katika madawati ya kijinsia yaliyowekwa polisi. "Ninapinga madawati haya kuwapo polisi kwa sababu kitendo cha mtu kutoka kwenda polisi kumshtaki mume wake au baba yake mdogo au mjomba wake ni jambo gumu na watu wanaogopa, elimu inahitajika hasa vijijini, tujiulize madawati ya kijinsia yapo je ni wangapi wanakwenda kuripoti," alihoji.

Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Lindi, Tecla Ungele, alisema idadi ya madawati yaliyopo hadi sasa ni kidogo huku kesi zikiwa nyingi na kuomba lifanyiwe kazi.

Mbunge wa Viti Maalum CHADEMA, Grace Tendega, aliomba wakati wa kutekeleza programu hiyo wasiwabague wanaume, wafundishwe ili wafahamu athari za kubaka.

Mbunge wa Viti Maalum CCM, Pauline Nahato, alisema mtoto anapofanyiwa ukatili upo uwezekano mkubwa baadaye akanyanyasa wengine kama hatasaidiwa kisaikolojia wakati wa ukuaji wake.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Aloyce Kamamba, alipongeza wizara kwa semina hiyo kwa wabunge ambayo imewanufaisha kwa mambo mengi na kuitaka kufanyia kazi maoni yaliyotolewa na wabunge.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaifa ya ushauri kuhusu utekelezaji wa ahadi za nchi kwenye jukwaa la kizazi chenye usawa, Angellah Kairuki, alisema masuala ya jamii yanamuhusu kila mmoja na kuna kila sababu ya kukemea ukatili unaoendelea.

"Kuna baadhi ya nchi ambazo zimejitokeza kutoa ushirikiano katika utekelezaji wa programu hii itakayozinduliwa mwezi Juni, wabunge programu hii ni yenu na itashuka hadi ngazi ya chini, tunaomba ushirikiano," aliwaomba.

# Chongolo awageukia wachimbaji madini

**Na Maulid Mmbaga,** SHINYANGA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo amewataka wachimbaji wadogo wa madini kuzingatia utunzaji wa mazingira na miundombinu kujiepusha kuchimba maeneo yaliyopita mabomba ya maji.

Alitoa wito huo jana katika Kijiji cha Mwakitolyo, Shinyanga Vijijini, baada ya kukagua ujenzi wa tangi la maji lenye lita za ujazo 500,000 unaogharimu zaidi ya Sh. milioni 394 na kuratibiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kahama-Shinyanga (KASHWASA).

Aliwapongeza wananchi wa eneo hilo kwa kutenga eneo la msitu wa hifadhi unaosaidia kupambana na mabadiliko ya tabianchi, huku akitoa wito kwa watu wa sehemu nyingine kutenga sehemu za uhifadhi kwa sababu zina tija kubwa kwa wananchi na taifa kwa ujumla.

"Sio kila eneo linatakiwa kuwa na ng'ombe, kuchimbwa na sio kila eneo linatakiwa kutumiwa kwa kila kitu, lazima muhifadhi maeneo machache kwa ajili ya matumizi maalumu ya uhifadhi ndani ya maeneo yenu.

"Niwaombe sana najua wengi wenu hapa ni wachimbaji wa madini, sehemu zinazopita mitandao ya maji na mabomba msiende kuchimba na kuyakatakata mabomba hayo, lindeni miundombinu hiyo ya maji," alisisitiza Chongolo.

Aliwakumbusha kuwa wananchi wa eneo hilo wanaongezeka kadri siku zinavyozidi kwenda na kuwataka watunze miundombinu ya maendeleo inayoendelea kutekelezwa katika maeneo yao kwasababu ina umuhimu kwa maisha yao pia inatija kwa mambo mbalimbali.

"Sasahivi mnafanya kazi ya kuvundika udongo ili mtoe dhahabu, kuvundika kule kunahitaji maji mkiichezea miundombinu maana yake hata kazi ya kutengeneza dhahabu kwa kuvundika udongo kwenye yale matangi haitaenda vizuri na matokeo yake mtarudi kwenye ulalamikaji," alisema Chongolo.

Aliipongeza Mamlaka ya maji KASHWASA kwa kutimiza wajibu wao na kuwasisitiza kuendelea kusimamia vizuri miradi na miundombinu wanayoitekeleza ili ilete matokeo.

Vile vile, aliitaka Mamlaka ya Usambazaji Maji na Usafi na Mazingira Vijijini (RUWASA), kuanza mapema kazi ya usambazaji wa maji ili wananchi wapate maji karibu na maeneo yao na waendelee kuendesha shughuli zao za kujipatia kipato.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, alisisitiza wananchi kujiandaa kuhesabiwa ili serikali inapowapelekea miradi ya maendeleo wapatiwe kulingana na idadi yao.

"Siku ya sensa msije mkakaa huko kwenye migodi, jitokezeni kwa wingi mhesabiwe, serikali itapeleka huduma kwa wananchi kwa kuzingatia idadi yao, kama hauko kwenye hesabu ina maana utakosa na hao ndiyo watakuwa wa kwanza kulalamika, mjitokeze idadi yenu ijulikane kwa maendeleo yenu na taifa kwa ujumla," alisema Sophia.



# Tumefungua Maombi ya Ufadhili wa Masomo na Mafunzo kwa Ushauri ya NMB Nuru Yangu kwa Mwaka 2022

Kwa Wanafunzi wanaoingia Kidato cha Tano na Elimu ya Juu

NMB FOUNDATION

## KUHUSU UFADHILI HUU

NMB Foundation imeanzisha mpango wa ufadhili wa masomo na mafunzo kwa ushauri kupitia program ya Nuru Yangu, yenye lengo la kuunga mkono sekta ya elimu, kupunguza umaskini na kuendeleza kizazi kijacho cha viongozi, kwa kuongeza wigo wa upatikanaji wa elimu ya sekondari na vyuo vikuu.

Tunatazamia kuchochea uwezo wa vijana wenye kiu ya maarifa, wanaotazamia kesho iliyo bora na wenye shauku ya kuleta mabadiliko ulimwenguni. Huu ni mpango wa masomo na ushauri unaolenga kuwanufaisha vijana wanaotoka katika familia zenye kipato cha chini wenye uwezo mzuri kimasomo na walio na bidii zenye kuleta matokeo chanya kwa maendeleo ya jamii yetu.

## Kidato cha Tano

Waombaji watakaofanikiwa watapatiwa ufadhili kamili, ambao utahusisha gharama zote za moja kwa moja zinazolipwa shuleni ikiwemo ada ya masomo, uniform ,vitabu ,madaftari ,nauli za kwenda na kurudi kwa walio kwenye shule za bweni, hela ya kujikimu (pale inapohitajika), pamoja na kadi ya matibabu ya NHIF na mahitaji mengine kama yalivyooanishwa kwenye fomu ya kujiunga na shule.

### VIGEZO VYA USTAHIKI

Ili kukidhi vigezo kwa ajili ya mpango wa **ufadhili wa masomo na programu ya ushauri ya Nuru Yangu** *(Nuru Yangu Scholarship and Mentorship Program)*, waombaji wote lazima wakidhi vigezo vyote vya ustahiki hapo chini:

1. Lazima uwe raia wa Tanzania ambaye umemaliza kidato cha nne mwaka 2021.
2. Uwe na matokeo bora katika mitihani ya kidato cha nne, (divisheni 1 point 7-14).
3. Lazima uwe umechaguliwa katika moja ya shule za umma, kwa masomo ya kidato cha tano 2022.
4. Lazima kuonyesha uhitaji wa kifedha.

**Nyaraka zinazohitajika kuambatanishwa na maombi;**

1. Barua ya maombi ikielezea kwanini upewe ufadhili
2. Barua ya udhamini kutoka ofisi ya Mtendaji Kata.
3. Nakala ya cheti cha kuzaliwa.
4. Nakala ya Cheti cha kifo (kama umefiwa na mzazi mmoja au wote).

### UTARATIBU WA MAOMBI

Tumefungua maombi ya ufadhili wa masomo na ushauri wa Nuru Yangu kwa mwaka wa masomo unaowahusu wanafunzi wanaoingia kidato cha tano mwaka 2022. Waombaji wote, ambao wanakidhi vigezo wanahimizwa kuomba kwa kujaza fomu inayopatikana kupitia **www.foundation.nmbbank.co.tz** au kwenye **tawi lolote la benki ya NMB**.

**Mwisho wa Kujisajili ni :**
**10 Juni 2022, 10:00jioni.**

## Elimu ya juu

Waombaji watakaofanikiwa watapatiwa ufadhili kamili, ambao utahusisha gharama zote za moja kwa moja zinazolipwa chuoni ikiwemo ada ya masomo, pamoja na gharama za mwanafunzi (chakula, malazi, vitabu na vifaa, mafunzo kwa vitendo na mahitaji muhimu ya kitivo) kama ilivyoainishwa katika muongozo wa gharama wa chuo. Mfadhiliwa pia atapatiwa kompyuta mpakato na mshauri atakaemsaidia kukua katika taaluma yake.

### MASOMO HUSIKA

Mpango huu wa ufadhili unalenga **kufadhili wanafunzi 50** kwa shahada za chuo za masomo mbalimbali yakiwemo:

- Business
- Oil and Gas
- Medicine
- Engineering
- Actuarial Science
- Computer Science or ICT
- Mathematics and Statistics
- Finance and Commerce
- Economics
- Data Science
- Data Mining
- Risk Management

** Masomo ambayo hayapo katika orodha iliyotajwa hapo juu, yatapata idhini kulingana na maamuzi ya NMB Foundation.*

### VIGEZO VYA USTAHIKI

Ili kukidhi vigezo kwa ajili ya mpango wa **ufadhili wa masomo na programu ya ushauri ya Nuru Yangu** (Nuru Yangu Scholarship and Mentorship Program), waombaji wote lazima wafikie vigezo vyote vya ustahiki hapo chini:

1. Lazima uwe raia wa Tanzania ambaye amemaliza Shule ya Sekondari (Kidato cha Sita).
2. Uwe na matokeo bora katika mitihani ya Kidato cha Sita Advanced Certificate of Secondary Education Examinations (ACSEE) divisheni 1 pointi 3-7.
3. Ufaulu mzuri katika matokeo ya kidato cha nne, divisheni 1 point 7-14 ni sifa ya nyongeza.
4. Lazima uwe na umri chini ya miaka 30.
5. Lazima uwe umechaguliwa katika moja ya chuo kikuu cha umma au taasisi ya juu ya umma inayotambulika, kwa masomo ya muda wote kwenye moja ya kozi zilizoainishwa kuwa sehemu ya program ya Nuru Yangu.
6. Lazima kuonyesha uhitaji wa kifedha.

**Nyakara zinazohitajika kuambatanishwa na maombi (zote ziwe zimehakikiwa)**

1. Nakala ya majibu au vyeti vya NECTA vya sekondari kidato cha nne na cha sita.
2. Nakala ya Cheti cha kifo (kama umefiwa na mzazi mmoja au wote).
3. Ushahidi/uthibitisho (kama umeonyesha kuwa na mahitaji maalumu katika fomu ya maombi)
4. Nakala ya cheti cha kuzaliwa.
5. Barua ya udhamini kutoka ofisi ya Mtendaji Kata.

### UTARATIBU WA MAOMBI

Tumefungua maombi ya ufadhili wa masomo na ushauri ya Nuru Yangu kwa mwaka wa masomo 2022/2023. Waombaji wote, ambao wanakidhi vigezo wanahimizwa kuomba kwa kujaza fomu inayopatikana kupitia **www.foundation.nmbbank.co.tz**

ANGALIZO 1: Hakikisha UNASOMA maagizo YOTE na unaelewa kabla ya kutuma maombi.

ANGALIZO 2: Hakikisha unajaza fomu ya maombi na kuikabidhi kwenye tawi la benki ya NMB lililokaribu na makazi yako. (kwa maombi ya kidato cha tano).

ANGALIZO 3: Hakikisha nyaraka zote zinazohitajika zinaambatanishwa na maombi yako yakiwa na taarifa sahihi, maombi yatakayokuwa na udanganyifu yataondolewa kwenye mchakato.

ANGALIZO 4: Sambamba na uombaji wa ufadhili wa programu ya chuo kikuu waombaji wanaimizwa kufanya maombi ya ufadhili wa Bodi ya Mikopo (HESLB). Hata hivyo, endapo muombaji atapata ufadhili wa program ya Nuru Yangu na HESLB, atatakiwa kujitoa kwenye udhamini wa HESLB pindi tu wapatapo ufadhili huu.

ANGALIZO 5: Waombaji wote wanaokidhi vigezo vilivyotajwa wana fursa sawa.

**Mwisho wa Kujisajili ni:**
**30 Septemba 2022, 10:00jioni.**

Elimu

**Kwa taarifa zaidi kuhusu maombi ya Nuru Yangu Scholarship and Mentorship Program:**
**Tutumie barua pepe: foundation@nmbbank.co.tz** au
**Tupigie kupitia namba: 0800 002 002**

***foundation.nmbbank.co.tz***

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TFF rudisheni Fainali FA Cup kwa Mkapa kuipa hadhi

**MWISHONI** mwa wiki zilipigwa nusu fainali mbili za Kombe la Shirikisho la Soka nchini, maarufu Azam Sports Federation Cup (ASFC) ama FA Cup, kwa msimu wa 2021/2022.

Nusu fainali ya kwanza ilipigwa Jumamosi katika Uwanja wa CCM Kirumba ambapo Yanga iliibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Simba na ya pili ikapigwa jana Jumapili kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha kati ya Azam FC na Coastal Union.

Kawaida michuano hiyo huanzia ngazi ya chini kwa kuchezwa katika viwanja mbalimbali kwa kutegemeana na droo inavyochezeshwa kabla ya kutinga raundi ya 64 ambapo timu za Ligi Kuu huanza kushiriki.

Michuano hiyo huanza kuwa na msisimko mkubwa na kuvuta hisia zaidi pindi timu za Ligi Kuu zinapoingia, hiyo ikitokana na kuwa na mashabiki wengi.

Hisia, wingi na utayari wa mashabiki huongezeka zaidi inapoingia hatua ya robo fainali, nusu fainali na hatimaye fainali, ambapo bingwa huiwakilisha nchi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Inapofika hatua ya nusu fainali na fainali, TFF hupanga viwanja vya mikoani nje ya ule mkubwa nchini wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, lengo likiwa zuri tu la kutaka kupeleka soka kila kona ya nchi hususan kwa mikoa ambayo haina timu za Ligi Kuu.

Tunaelewa kabisa lengo la TFF ni zuri kwani linalenga kuchochea wadau wa mchezo huo kwenye mikoa hiyo kuona haja ya kuwa na timu za Ligi Kuu ili kupata burudani ya soka mara nyingi zaidi kwa msimu.

Lakini pamoja na lengo zuri kwa TFF, sisi tunaona ipo haja kwa sasa shirikisho hilo kubadiki utaratibu huo na kufanya kuwa kuanzia timu za Ligi Kuu zinapoingia michuano hiyo kupangwa kuchezwa viwanja vya mikoani ambazo hazina timu Ligi Kuu na inapofika hatua ya nusu fainali na fainali, kurejeshwa katika uwanja ulio bora zaidi nchini, Benjamin Mkapa.

Lakini pia kama inaona katika hatua za awali pindi zinapoingia timu za Ligi Kuu ni vigumu kufanya hivyo, basi TFF inaweza kulifanya kuanzia hatua ya robo fainali ili kufikia malengo ambayo inaona yanaweza kutimia wakifanya hivyo. Tunaona michuano hiyo inapofika hatua ya nusu fainali, inapaswa kuchezwa katika viwanja bora viwili nchini, kwa nusu fainali moja kupigwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi na nyingine Benjamin Mkapa. Na hatua ya fainali ipigwe tena kwa Mkapa.

Tunasema hivyo, kwa sababu hatua hizo huvutia watu wengi zaidi kutaka kwenda uwanjani kushuhudia mubashara, lakini pia mechi kubwa kama za hatua hiyo, ndizo hutangaza soka letu pamoja na ubora wa miondombinu tuliyonayo nchini kisoka.

Tunatambua wapo watakaohoji kuwa mbona uwezo wa Uwanja wa Azam Complex nao ni mdogo, lakini hapa tumeutaja kwa kuakisi zaidi ubora wake hasa tukizingatia kuwa zipo timu kutoka nje zimekuwa zikiomba nafasi ya kuja kucheza mechi zake za kimataifa hapo na kuiingizia nchi fedha za kigeni.

Kupeleka mechi kubwa kama hizo, ambazo zinafuatiliwa na wapenda soka wengi ndani na nje ya nchi, ni kuinyima fursa Tanzania kutangaza ubora wa miondombinu ya viwanja vyetu hivyo ambavyo vinaweza kuingizia nchi mapato ya fedha za kigeni.

Lakini pia, mechi kama hiyo ambayo huvuta hisia kubwa ya mashabiki, tunaamini kwamba waliohudhuria uwanjani hata waliokuwa wakifuatikia kupitia TV hawakutendewa haki kutokana na ubovu wa uwanja, mpira kuonekana ukidundadunda jambo ambalo linapoteza raha ya mechi kubwa.

Kuiga jambo jema si dhambi, hivyo TFF haina budi kuiga ama kufuata utaratibu kama wa England ambapo michuano hiyo ya FA na ile ya Kombe la Ligi (Carabao Cup), fainali mechi hizo hupigwa Uwanja wa Wembley (Taifa).

Pamoja na England kuwa na viwanja vingi bora, hufanya hivyo, kwanza kwa sababu Wembley ni Uwanja huru (Neutral Ground), ubora na ukubwa, lakini pia hutumia fursa hiyo kuutangaza na kutangaza soka lao.

Hivyo, ni wakati sasa kwa TFF kubadili mtazamo wake huo na kutotazama faida moja tu kwenye michuano hiyo, ili kuleta ufanisi bora zaidi na mapinduzi makubwa katika soka letu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Hongera Yanga, Simba sasa tengenezeni timu

**UNAWEZA** kusema huu ni msimu wa Yanga, kwa sababu kila inachokifanya kinakubali. Mbali na uongozi imara, lakini ina kikosi bora, ambacho pia kimechangamka na bahati kubwa msimu huu.

Kwa sasa ni kama ipo varandani ikielekea chumbani kutwaa ubingwa wa Tanzania Bara, baada ya kupita misimu minne migumu katika mataji nchini.

Juzi imeivua rasmi Simba ubingwa wa Kombe la FA kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza kwa kuifunga bao 1-0, ikielekea fainali ya Kombe la FA.

Ukitazama mfululizo wa mechi za Yanga, unaweza kuipa asilimia kubwa ya kwenda kutwaa pia ubingwa wa Kombe la FA, kwa sababu mpaka sasa inabaki kuwa timu pekee ambayo haijafungwa ukijumlisha michuano yote miwili, Ligi Kuu Tanzania na Kombe la FA.

Unaona wachezaji wake wanapocheza wana ari, nguvu na uwezo mkubwa wa kupambana, pamoja na wachezaji wanaojua kukaa na mpira mguuni.

Moja kati ya mambo ya kupongezwa kwa Yanga msimu huu ni usajili walioufanya ambao mwanzo ulibezwa na baadhi ya watu, wakidhani kwamba kila mwaka inaweza kuwa hivyo hivyo.

Ni baada ya klabu hiyo kupitia kipindi kigumu ikisajili wachezaji ambao ama hawakuwa na uwezo wa kuichezea timu hiyo, au hawakuwa wakifiti kwenye mfumo wa timu hiyo.

Msimu huu imesajili baadhi ya wachezaji waliokuja kukibadilisha kabisa kikosi hicho na kukifanya kuwa cha kuogopwa kama Fiston Mayele, Djuma Shaaban, Yannick Bangala, Dickson Job, Djigui Diarra, Khalid Aucho na wengineo.

Imekuwa ni Yanga ambayo baada ya miaka mingi imeondokana na ule mfumo wake wa enzi na enzi wa kutumia mawinga asili na krosi kwa ajili ya kushambulia, badala yake sasa inatumia viungo wa kati kutengeneza mashambulizi, kitu ambacho ni aghalabu sana kukiona kwa utamaduni wa klabu hiyo. Ndiyo maana kwa sasa Yanga imekuwa ikichezea sana mpira, hasa katikati, mfumo ambao ni asili ya klabu ya Simba, ambayo msimu huu haina.

Kutokana na jinsi Yanga ilivyokuwa inacheza tangu kuanza kwa msimu huu, ingekuwa soka halitendi haki kama isingepata taji lolote, ile ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania au Kombe la FA, au vyote kwa pamoja.

Nitoe pongezi kwa uongozi wa klabu hiyo, lakini pia nikitoa angalizo kuwa ikomae kwenye michuano ya kimataifa, kwani inakwenda kucheza Ligi ya Mabingwa, hivyo ubabe inaouonyesha nchini ikauonyeshe huko.

Haipendezi kuona klabu kubwa kama Yanga ikipambana na kina Dodoma Jiji kila msimu, badala ya kina Asec Mimosas, TP Mazembe, Al Ahly, Raja Casablanca, Esperance na nyinginezo.

Kwa upande wa Simba, nadhani wachezaji wake wengi tayari hawana wanachotafuta, kwani kila walichokuwa wanakitaka wamekipata.

Wengi wa wachezaji wao ni wale wa tangu 2017, ambao walitengeneza msingi na kuanza kutwaa ubingwa misimu minne mfululizo.

Ilichokuwa ikikifanya Simba ni kuwaongezea wachezaji watatu wanne, lakini kulikuwa na msingi wa wachezaji kina Mzamiru Yassin, Aishi Manula, Mohamed Hussein, John Bocco, Erasto Nyoni na wengineo.

Wengi wao sasa viwango vimeporomoka, wengine umri umekwenda, lakini wapo ambao hawana vyote hivyo, lakini wamebweteka na ushindi wa misimu yote ambayo timu imekuwa ikiupata. Ukitazama kwa sasa wachezaji wa Simba wengi hawapambani, wanacheza kama michuano ya bonanza na si mashindano.

Nimemsikia Rais wa Heshima na Mwekezaji wa klabu hiyo, Dk. Mohamed 'Mo' Dewji, akiitaka Bodi ya Wakurugenzi ya klabu hiyo ifanye maamuzi magumu.

Ni kweli, inahitaji ifanye usajili mkubwa ambao utaanza kuweka msingi mpya, ili hata msimu ujao wawe wanajazia tu wachezaji watatu wanne au watano.

Inashangaza kuona wachezaji wa Simba hawawezi kuwanyang'anya wachezaji wa timu pinzani mpira. Hii si kwenye mechi ya Yanga tu, bali tangu msimu unaanza. Wanaonekana hawana stamina, lakini pia kila wanapogongana na wachezaji wa timu pinzani wanaumia wao.

Nadhani maamuzi magumu yaanzie kwenye benchi la ufundi, hasa kocha wa viungo na utimamu wa mwili, baada ya hapo ndipo usajili uanze kwenye maeneo yote.

Ukiitazama Simba ina mapungufu maeneo yote, pembeni, kati, viungo wa kukaba, kushambulia na kutoa pasi za mabao, pamoja na mastraika. Kifupi ni kama vile imetengeneza timu mpya.

HABARI KITAIFA




Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema (Kushoto), Mstahiki Meya wa Manispaa ya Shinyanga, Elias Ramadhani (katikati) na Mkuu wa Matawi ya Benki ya Exim, Agnes Kaganda (kulia) wakiwa wameketi kwenye moja ya madawati 100 yaliyotolewa na benki ya Exim Tanzania. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TaFF yatoa ruzuku bilioni 38/-

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MFUKO wa Misitu Tanzania (TaFF), kwa miaka kumi umetoa ruzuku ya jumla ya Sh. bilioni 38.6 kugharamia miradi 738 yenye mchango kwenye ulinzi, uhifadhi, usimamizi na uendeshaji wa rasilimali misitu.

Katibu Tawala wa Mfuko huo, Dk. Tuly Msuya, alisema hayo mjini hapa kuwa mfuko huo ulizinduliwa mwaka 2009/2010 na ulianza rasmi utekelezaji wa majukumu yake Julai 2011.

Alisema Mfuko wa Misitu Tanzania unawezesha wananchi kiuchumi kupitia utoaji wa ruzuku kugharamia miradi ya uhifadhi, usimamizi, uendelezaji na matumizi endelevu ya rasilimali misitu katika mikoa ya Tanzania.

Katibu Tawala wa Mfuko huo alisema, kuanzia mwaka wa fedha 2020/2021, ulianzisha programu maalumu ya kutoa ruzuku kwa shule za msingi na sekondari kwa ajili ya kuanzisha vitalu, ili kupata miche ya miti ya kupanda katika maeneo ya shule na kupatiwa wanafunzi kupanda katika maeneo ya makazi yao.

Alifafanua kuwa katika mwaka huo wa fedha, mfuko ulitoa ruzuku ya jumla ya Sh. milioni 299.9 kwa shule 60 kutoka wilaya 25 za mikoa sita yenye mazingira ya ukame kwa ajili ya kutekeleza miradi ya uanzishwaji wa vitalu vya miti na upandaji miti shuleni.

Alisema mwaka wa fedha wa 2021/2022, mfuko ulitoa ruzuku ya jumla ya Sh. milioni 315 kwa shule 63 katika mikoa minane ukiwamo wa Dodoma katika wilaya mbili za Chamwino na Dodoma.

Mingine ni Singida, Shinyanga, Kagera, Manyara, Arusha, Kilimanjaro na Simiyu.

"Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023, mfuko unatarajia kutoa Sh. milioni 370 kwa miradi ya shule 74 katika wilaya 37 ya mikoa 12," alisema Dk. Msuya.

Kwa upande wake, Ofisa Elimu Taaluma wa Wilaya ya Chamwino, mkoani Dodoma, Happiness Mgongo, alisema wilaya imenufaika kwa kupata ruzuku kwa shule nne na kila moja imepatiwa Sh. milioni 10 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya uanzishwaji wa vitalu na upandaji miti shuleni.

Alizitaja shule za wilaya hiyo zilizonufaika ni shule ya msingi Idifu, Loje, Mvumi Misheni na Shule ya Sekondari Makang'wa.

Alisema shule sita zimenufaika kwa kupatiwa fedha za ruzuku ambazo ni Shule ya Msingi Ihumwa, Iyumbu, Medeli, Mkapa, Mnadani na Nala.

# TRA yahimiza wananchi kuhakiki ubora vinywaji

**Na Gwamaka Alipipi**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), imewataka wananchi kuhakiki ubora wa vinywaji kabla ya kutumia ili kulinda afya zao.

Wito huo umetolewa jana na Meneja Mradi Stempu za Kodi za Kielektroniki (ETS) kutoka TRA, Innocent Minja, wakati wa mafunzo ya Kampeni ya "Hakiki Stempu, Linda Afya Yako."

Kampeni hiyo imezinduliwa hivi karibuni na TRA na imewekeza na kufanya maboresho makubwa katika mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), ikiwa na lengo la kuongeza ufanisi, uwajibikaji, uwazi na kurahisisha ukusanyaji wa mapato serikalini.

Minja alisema dhumuni la mafunzo hayo ni kuuhabarisha umma wa watumiaji wa bidhaa, eneo mojawapo ambalo maboresho hayo yamefanyika ni katika stempu hizo.

Minja alisema ETS ni alama maalum zinazobandikwa au kuchapishwa katika bidhaa ili kuonesha kuwa ni halali na imezalishwa au kuingizwa nchini na mfanyabiashara anayetambulika, amelipa kodi ya ushuru wa bidhaa stahiki.

Alisema mfumo huo umeunganishwa na TRA ili kupata takwimu sahihi za uzalishaji, uagizwaji kwa maana ya idadi, ujazo pamoja na kodi halisi inayostahili kutozwa.

"TRA inapenda kuwahamasisha wananchi wanaotumia bidhaa hizo kushiriki kulinda afya zao kwa kutambua bidhaa halisi na halali kwa matumizi yao."

Aliwaomba wananchi kutumia simu zao za kiganjani kutambua bidhaa halali wanazotaka kuzitumia na watumiaji wanaweza kuzitambua kuwa halali kabla ya kuzitumia kwa kupakua App ya Hakiki Stempu kwenye simu zao bure.

"Kwa sasa bidhaa zinazobandikwa stempu za kielektroniki za ushuru ni sigara, mvinyo wa zabibu, pombe kali, bia, mvinyo wa matunda mengine kama vile ndizi, rozela, nyanya pamoja na aina zote za vileo," alisema Minja.

Alitaja bidhaa zingine ni vinywaji laini kama soda, visisimuzi, sharubati, maji na bidhaa za muziki na filamu zilizofungashwa kwenye CDs/ DVDs/ kanda.

Minja alisema hadi sasa viwanda ambavyo vimeunganishwa na mifumo ya ETS nchini ni 286 na waagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi ni 106.

# 390 waliokatisha masomo kwa ujauzito, utoro warejea shuleni

**Na Ibrahim Yassin,** TUNDUMA

WANAFUNZI 390 wa shule mbalimbali za sekondari katika Halmashauri ya mji Tunduma waliokatisha masomo kwa kupata ujauzito na utoro, wameanza kurejea shule.

Hatua hiyo imetokana na kauli ya Rais Samia Suluhu Hassan, kuagiza wanafunzi waliopata ujauzito warejee shule baada ya kujifungua.

Kasi ya wanafunzi kupata ujauzito imeendelea kutokana na mji wa Tunduma kuwa wa kibiashara huku wazazi wengi wakiwa wameegemea zaidi shughuli za kutafuta fedha na kusahau kufuatilia nyendo za watoto wao ambao wanatumbukia kwenye vishawishi.

Kauli ya Rais Samia imewaibua wazazi wengi na kumpongeza wakisema amefanya jambo la muhimu huku wakijipanga kuhakikisha wanakuwa wazazi wema kwa kuwafuatilia watoto wao ili kutimiza ndoto zao.

Judith Msari, mmoja wa wanafunzi walioacha shule baada ya kupata ujauzito, alisema aliupata akiwa kidato cha tatu mwaka 2020 na baada ya kauli ya Rais Samia ameamua kurejea darasani akirudia kidato cha pili.

Alisema yeye ni mmoja wa waathirika na kuiomba serikali iharakishe ujenzi wa mabweni ili wanafunzi wa kike waweze kulala shuleni badala ya kwenda na kurudi kwa kuwa wengi wao wanatoka mbali na matokeo yake ni kurubuniwa na wanaume hasa waendesha bodaboda na madreva wa malori.

Nelly Jobu, wa kidato cha tano Chisunga Sekondari, alisema tatizo la ujauzito kuwakumba wanafunzi katika shule za halmashauri ya Tunduma ni umaskini na malezi duni ya wazazi au walezi, hali inayowafanya watoto kutumbukia kwenye vishawishi vya kimapenzi na kujikuta wakipata mimba.

Alisema miaka ya hivi karibuni kulikuwapo na ukosefu wa ajira na wahitimu wa vyuo mbalimbali walikuwa wakizagaa mitaani bila kupata ajira licha ya wazazi wao kutumia fedha nyingi kuwasomesha.

Hali hiyo alisema iliwakosesha moyo wa kusoma wakidhani hata wao watakuwa mitaani wanapomaliza masomo.

Mkurugenzi wa shule binafsi ya Sekondari Chisunga, Mwalimu Joent Chisunga, alisema baada ya agizo la Rais, alipokea wanafunzi wengi na tayari wengine wameenda vyuo vikuu kwa kuwa katika shule yake wanasoma masomo ya miaka miwili (QT) halafu wakifanya vizuri katika mitihani yao wanaenda shule za serikali hadi vyuo vikuu.

Alisema ndani ya miaka miwili amepokea wanafunzi 419 kati ya hao, wasichana 317 ambao waliacha shule kwa kupata ujauzito na wavulana waliacha kwa sababu mbalimbali ikiwamo utoro.

Hivi sasa alisema wanafunzi 44 wamefanya mitihani ya kidato cha sita na ana uhakika kuwa watafaulu mitihani yao.

"Ninampongeza Rais Samia kwa kuruhusu wasichana walioacha shule kwa kupata ujauzito ama utoro kurejea shule, tunashirikiana vizuri na halmashauri kupitia idara ya elimu sekondari kwa kuwa wanafunzi tunaowapokea tunawapa masomo maalum kuhakikisha wanakuwa na mwendelezo mzuri," alisema.

Akizungumzia maboresho kuondoa msongamano wa wanafunzi darasani, Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Fillimoni Magesa, alisema wamepokea Sh. 1,266,339,776 kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa na ukarabati shule chakavu.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Ayoub Mlimba, alisema Tunduma ni halmashauri ya kimkakati na imekuwa na idadi kubwa ya watu kutokana na kuwa lango kuu la nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) na kukumbwa na idadi kubwa ya upungufu wa madarasa na madawati.

Alisema serikali ilisikia kilio chao kwa kuwapa fedha nyingi zinazowasaidia kujenga shule mpya zikiwamo za ghorofa, moja ni ya sekondari na nyingine shule ya msingi.

# Warioba atoa ushauri uhaba mafuta ya kula

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

WAZIRI Mkuu mstaafu, Joseph Warioba, amewaagiza watafiti wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), kufaya utafiti wa mimea mingine inayoweza kuzalisha mafuta ya kula ili taifa liondokane na tatizo la bidhaa hiyo inayoagizwa kutoka nje.

Jaji Warioba ambaye ni Mkuu wa Chuo, alisema imefika wakati watafiti kulisaidia taifa kwa kuwa na mafuta yatakayozalishwa nchini ikiwa ni hatua ya kuunga mkono juhudi zinazofanywa na serikali kuondokana na utegemezi wa mafuta kutoka nje.

Alitoa maelekezo hayo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza na watumishi wa chuo kikuu hicho katika kampasi ya Edward Moringe baada ya Makamu Mkuu wa Chuo, Profesa Raphael Chibunda, kutoa taarifa ya majukumu ya chuo hicho.

Alisema kwa sasa nchi inakabiliwa na changamoto ya mafuta ya kula, hali iliyosababishwa na mabadiliko duniani ikiwamo vita ya Ukraine na Russia na kwamba wakati huu ndiyo muafaka kwa watafiti kuisaidia nchi.

Alisema Tanzania imebarikiwa kuwa na mimea mingi inayoweza kutoa mafuta, akitolea mfano alizeti, michikichi, nazi na mimea mingine inayoweza kuwa na mafuta.

"Tukiachilia kupanda kwa bei ya mafuta ya petroli, lakini ilianza mafuta ya kupikia na ukiona duniani vyanzo vya mafuta haya vilianza kuwa na matatizo hata kabla ya vita hiyo kuanza hivyo lazima kupitia watafiti wetu tusaidie nchi kuondokana na changamoto hizo," alisema Jaji Warioba. Alisema kutokana na changamoto hiyo serikali imeonesha juhudi ya kutaka kuendeleza eneo hilo ili taifa lisiwe tegemezi wa mafuta ya kula nchini.

Vile vile, alisema serikali inajitahidi kuongeza nguvu kwenye maeneo ya maendeleo kama kilimo na kwamba kutokana na mabadiliko mbalimbali sekta hiyo haijafanya vizuri.

Alisema SUA ina watafiti waliobobea kwenye utafiti utakaochangia na kuboresha mbinu za kuboresha kilimo katika kujitosheleza kwa chakula na mafuta.

Aidha, aliwakumbusha wasomi hao kuwa serikali inafumua mfumo wa elimu na kwamba wana wajibu wa kushiriki kutoa maoni yao ili kuwa na elimu itakayowatengenezea ajira badala wanaosubiri kuajiriwa.

Alisema licha ya changamoto zinazokikabili chuo hicho, kuna mafanikio makubwa ndani ya miaka mitano kama uboreshaji wa miundombinu, ukarabati wa majengo ya zamani na ujenzi wa mengine mapya likiwamo la maabara mtambuka.

Awali, Makamu Mkuu wa SUA, Profesa Raphael Chibunda, alisema chuo hicho kinafanya vizuri katika nyanja za utafiti kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo kutoka ndani na nje ya nchi, ambazo zilichapishwa kwenye majalada ya kitaifa na kimataifa kati ya 200 -250 kupitia miradi isiyopungua 120 kwa mwaka yenye thamani ya Sh. bilioni 25.

Alisema katika miaka ya hivi karibuni mwelekeo wa SUA umekuwa ni kukuza matumizi ya Sayansi, Teknolojia na Elimu Bunifu.



Watendaji kutoka Idara na Taasisi za Wizara ya Ardhi na Makamishna wa Ardhi Wasaidizi wa mikoa wakimsikiliza Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Dk. Angeline Mabula (hayupo pichani). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mabula ataka 'clinic' ardhi kutatua migogoro

**Na Munir Shemweta,**
DODOMA

WAZIRI wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amewataka Makamishna wa Ardhi Wasaidizi wa mikoa nchini kuanzisha 'Clinic' za Ardhi kushughulikia changamoto za sekta ya ardhi katika mikoa yao.

"Mjiwekee utaratibu mzuri wa kusikiliza changamoto za ardhi katika mikoa yenu kwa kuanzisha kliniki za ardhi, Mwanza wamekuwa wakifanya hivyo na wamefanikiwa," alisema.

Alisema kuna changamoto ya kutokuwa makini kwa watendaji na kutoa mfano wa barua za malalamiko zinazokwenda kwenye ofisi yake kuwa zingeweza kushughulikiwa katika mikoa husika.

"Changamoto kubwa hatuko serious, barua za malamimko ya migogoro ya ardhi zinakuja kwa waziri na mimi nazirudisha kwenu kupata ufumbuzi na huko napata majibu why (kwanini) msingeshughulikia mpaka zije huku? Ndiyo maana migogoro inakuwa mingi," alisema Mabula.

Alisema hayo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza na Wakuu wa taasisi zilizo chini ya wizara, Makamishna wa Ardhi Wasaidizi wa mikoa na watendaji wa Makao Makao Makuu baada ya kupitishwa kwa bajeti ya wizara yake na Bunge ya Sh. 110,323,474,000 ziliidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Dk. Mabula, alisema sehemu kubwa ya migogoro ardhi inachangiwa na kutokuwapo mipango ya matumizi bora ya ardhi kwenye halmashauri na kuwataka Makamishna wa Ardhi Wasaidizi wa mikoa kuzikumbusha halmashauri katika mikoa yao kutenga fedha kwa ajili ya mipango hiyo.

Pia, aliwataka kuhakikisha pesa za halmashauri zinazokopeshwa kwa ajili ya miradi ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa na ile faida inayopatikana itumike kuboresha sekta ya ardhi.

Kuhusu urasimishaji makazi holela, aliwataka Makamishna wa Ardhi Wasaidizi wa mikoa kuhakikisha kampuni zilizoshindwa kukamilisha kazi za urasimishaji zinachukuliwa hatua na kuangalia namna bora ya kukwamua kazi zilizokwama.

"Kama wao wamekwama kukamilisha kazi za urasimishaji ninyi mnafanyaje? Undeni timu katika mikoa kwenda wilaya moja hadi nyingine kulingana na mahitaji, zoezi hili lina chanagamoto kubwa sana mfano Mkoa wa Tabora umefanya vizuri sana," alisema Dk. Mabula.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete alikemea ucheleweshaji hati kwa wamiliki wa ardhi na kueleza kuwa, kama kuna tatizo linalosababisha mwananchi kutopata hati yake haraka basi aelezwe badala ya kumuacha mpaka aanze kulalamika.

"Kuna kilio cha wananchi hati kuchukua muda mrefu, nina mfano wa Dar es Salaam kuna mama mmoja hati yake ilichukua miaka saba na tatizo lake ilikuwa kitambulisho cha NIDA, lakini hakuelezwa hadi akaja kulalamika kwangu, kama lipo tatizo mhusika aelezwe mapema, maduhuli yanakosekana kutokana na wananchi kutopewa hati," alisema Ridhiwani.

Dk. Allan Kijazi, Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi alieleza kuwa, ipo changamoto kwa baadhi ya watumishi kufanya kazi bila kufuata taratibu na taarifa zao hazitolewi na Makamishna wa Ardhi wa mikoa husika jambo alilolieleza linasababisha wizara kupata taarifa kupitia vyanzo vingine.

"Kuna changamoto ya watendaji kufanya kazi bila kufuata taratibu na taarifa hazipatikani na pale zinapopatikana ni kutoka other sources sasa utendaji wenu utapimwa pia na jinsi unavyosimamia watendaji wako," alisema Dk. Allan Kijazi.

## Mtendaji Mkuu NMB ashinda Tuzo Ubora Afrika 2022

**Na Mwandishi Wetu**

OFISA Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna, ametangazwa mshindi wa Tuzo ya Ofisa Mtendaji Mkuu Bora Afrika kwa mwaka 2022 (Tanzania) katika kipengele cha benki na uongozi jijini Nairobi, Kenya.

Tuzo hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Julias Alego Mkurugenzi Mtendaji Taasisi za Benki nchini Kenya na kupokelewa na Mweka Hazina Mkuu wa benki ya NMB, Aziz Chacha.

Akipokea tuzo hiyo kwa niaba ya ofisa huyo, Chacha alisema wanajisikia fahari na heshima kupokea tuzo hiyo.

"Ni heshima kubwa sana kuwa nanyi usiku wa leo kupokea Tuzo ya "African Banking CEO of the Year 2022 (Tanzania)" kwa niaba ya Ruth Zaipuna, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NMB Plc," alisema.

Aziz pia aliwashukuru wafanyakazi wa NMB kwa kujitolea kwao na nia ya kuendelea kuwa mstari wa mbele katika uvumbuzi, kuzingatia wateja, uthabiti, uaminifu, na usalama.

"Kwa maneno ya Ruth, natoa tuzo hii maalum kwa moja ya mtaji wetu mkubwa ambao ni wafanyakazi wa benki ya NMB ambao bila wao, pengine tusingekuwa hapa tulisherehekea," aliongeza.

Alibainisha kuwa benki yake kwa miaka mingi imekuwa na mchango mkubwa katika kusaidia shughuli mbalimbali za kiuchumi katika sekta nyingi ikiwamo Utalii, elimu, kilimo, miradi ya kimkakati ya muda mrefu na afya.

"Ninatoa tuzo hii kwa wadau wa benki ya NMB ambao wamejitolea kikamilifu katika azma yetu ya kubaki kweli bila kulinganishwa - benki imekuwa mstari wa mbele kwenye suala zima la ubunifu kwa kuzingatia wateja, uthabiti, uaminifu, usalama na usalama."

Zaipuna pia alitajwa kuwa miongoni mwa wanawake 74 wenye ushawishi mkubwa barani Afrika katika sherehe za wanawake wanaofanya biashara kubwa barani Afrika na data zilizotumika kutengeneza orodha hiyo ilitolewa kutoka Bloomberg na taarifa ya Africa.com.

Orodha hiyo iliwakilisha wanawake wanaofanya biashara kubwa barani Afrika. Biashara zote zinazoendeshwa na wanawake zenye mapato ya Dola za Kimarekani milioni 100 au zaidi.

Viongozi wengine wanawake walitajwa, ni pamoja Natascha Viljoen, Ofisa Mkuu Mtendaji wa kampuni ya Anglo American Platinum, Nompumelelo Thembekile Madisa, Ofisa Mkuu Mtendaji wa Bidvest Group na Leila Fourie, Mtendaji Mkuu wa Soko la Hisa la Johannesburg.

Viongozi wengine wanawake wa Afrika Mashariki kwenye orodha hiyo ni pamoja na Mitwa Ng'ambi, Ofisa Mtendaji Mkuu wa MTN Rwanda Telecommunications, Kendi Ntwiga-Nderitu, Mwakilishi wa kampuni ya Microsoft nchi, Kenya na Brenda Mbathi, Mkurugenzi wa kampuni ya General East Africa.

# Watoto 112,000 wanufaika mpango elimu bora

**Na Richard Makore,** SENGEREMA

WATOTO 112,000 kutoka mikoa mbalimbali nchini wananufaika na mpango wa elimu bora na ulinzi kwa vijana unaoratibiwa na shirika lisilo la kiserikali la kimataifa la Compassion Tanzania kwa kushirikiana na wafadhili kutoka Uholanzi kupitia makanisa washirika 500.

Akizungumza katika hafla iliyokutanisha waumini wa Kanisa la Africa Inland Church Tanzania (AICT), kutoka wilayani Sengerema, mkoani Mwanza, Mkurugenzi wa Shirika hilo, Mary Lema, alisema lengo la kukutana pamoja na wazazi na wafadhili kutoka nchini Uholanzi ni kukusanya zaidi ya Sh. milioni 300 ili kusaidia watoto wenye uhitaji.

"Leo tumejumuika pamoja na watoto, wazazi na marafiki zetu 30 kutoka Uholanzi kwa kufanya mazoezi ya kutembea, kukimbia pamoja na kuendesha baiskeli kwa lengo la kukusanya Sh. milioni 300 ambazo zitasaidia kujenga madarasa ya wanafunzi na kutoa elimu bora kwa watoto hao wenye uhitaji," alisema.

Alisema shirika lake linajihusisha na utoaji wa elimu, makuzi, malezi a ulinzi wa watoto na vijana katika mikoa mbalimbali hapa nchini.

Aliongeza kuwa watoto zaidi ya 112,000 wamenufaika na mpango huo ambao wanaufanya kwa kushirikiana na makanisa 500.

"Leo tupo hapa na wajumbe kutoka shirika hili ambao wanatoka nchini Uholanzi waliokuja nchini kuungana na sisi ili kuhakikisha tunapata fedha za kutekeleza mpango huu," alisema Mary.

Kwa upande wake, Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la AICT, Sengerema, Amos Ndangwaa, alisema mpango huo utasaidia wanafunzi 190 katika eneo hilo.

"Tumekuwa na huu mpango wa kusaidia watoto tangu mwaka 2008 na tuliandikisha watoto 200, lakini kwa sasa wamebaki watoto 190 kutokana na wengine kuhamishwa na wazazi wao pindi wanapohama makazi, lakini mpango huu umewasaidia sana kukuza elimu yao pia na wazazi kupunguza mahitaji katika kusomesha watoto wao, tumejengewa madarasa, wapo walimu wazuri na elimu nzuri inatolewa kwa watoto hawa," alisema.

Verendiana Venance, mzazi mwenye mtoto anayenufaika na mpango huo, eneo la Mlimani alisema mpango huo umesaidia mtoto wake kupata elimu.

"Nafurahi kupitia mpango huu unaoratibiwa na shirika la Compassion umemfanya mwanangu anapata elimu pamoja na maadili mema kwa kuwa hatukuwa na uwezo wa kumpleka shule," alisema.




Mke wa Makamu wa Rais, Mama Mbonimpaye Mpango (Mwenye kiremba cha rangi ya bluu) akisikiliza maelezo kutoka kwa wawezeshaji wa maabara ya hedhi salama mkoani Kigoma wakati wa maadhimisho ya Siku ya Hedhi Salama Duniani mwishoni mwa wiki. **PICHA: OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# Bilioni 100/- kujenga bandari Uvuvi Kilwa

**Na Mbaraka Kambona,** KILWA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki amewataka wananchi hususan wanaoishi wilayani Kilwa kujipanga kutumia vyema fursa zitakazojitokeza wakati wa utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Bandari ya Uvuvi utakaoanza mwezi Juni, mwaka huu.

Waziri Ndaki alitoa wito huo alipofanya ziara ya kutembelea na kukagua eneo lililotengwa kwa ajili ya ujenzi wa bandari hiyo lililopo wilayani Kilwa, mkoani Lindi, mwishoni mwa wiki.

Wakati akiongea na wananchi wa wilaya hiyo, alisema kuanza kwa ujenzi wa mradi huo kutaambatana na fursa mbalimbali zitakazo kuwa na manufaa kwao na kwamba ni vyema wananchi hao wakaanza kujiandaa ili mradi utakapoanza waweze kuwa sehemu ya wanufaika na sio watazamaji.

Alisema katika kuhakikisha mradi huo unajengwa na kukamilika, Rais Samia Suluhu Hassan ameridhia kutengwa kiasi cha pesa kisichopungua bilioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa bandari hiyo. "Naomba muiamini serikali ya Mama yetu makini, Rais Samia Suluhu Hassan, amedhamiria kujenga Tanzania, huu ni mradi wake wa kielelezo, wa kimkakati na utakaoacha alama kwenye nchi hii," alisema.

Waziri Ndaki aliwahakikishia wananchi wa Kilwa kuwa bandari hiyo itaanza kujengwa mapema mwezi Juni mwaka huu na aliwataka kujiandaa kuchangamkia fursa mbalimbali zitakazojitokeza wakati mradi huo unatekelezwa.

Awali, akitoa taarifa ya wilaya ilivyojiandaa kuhakikisha mradi huo unajengwa, Mkuu wa Wilaya ya Kilwa, Zainab Kawawa, alisema wameshafanya matayarisho yote kuhakikisha mradi huo unajengwa na wanaotakiwa kuachia maeneo yao kupisha mradi huo wapo tayari kufanya hivyo.

"Tunaamini kwamba bandari hii ya kimkakati itakapojengwa na kukamilika italeta tija kubwa kwa wavuvi na wananchi kwa ujumla na sisi tumeshafanya matayarisho yote ili mradi huu usikwame," alisema.

Naye, mvuvi anayefanya shughuli zake wilayani Kilwa, Suleiman Mohammed, akizungumza kwa niaba ya wenzake alisema ni kweli wanavuna samaki katika Bahari ya Hindi, lakini hawana sehemu ya uhakika ya kuuzia samaki wao kwa kuwa soko lililojengwa kwa ajili ya shughuli hiyo mpaka sasa halijaanza kutumika.

"Tunakuomba Mheshimiwa waziri soko hili lililojengwa lifanye kazi ili tuweze kulitumia kufanya biashara zetu," alisema Mohammed. Waziri Ndaki aliwataka wananchi wanaotakiwa kuachia maeneo yao kwa ajili ya kupisha mradi huo wasiwe na wasiwasi, serikali itahakikisha kila mmoja anapata haki yake anayostahili.

# Ongezeko bili za maji chanzo kutokaguliwa dira

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MALALAMIKO ya kupanda kwa ankara za maji kwa watumiaji wa huduma hiyo mkoani Shinyanga, inadaiwa kusababishwa na kutokaguliwa kwa dira za maji (mita) kabla ya kufungia wateja na Wakala wa Vipimo (WMA) na wateja kuendelea kulipa gharama kubwa.

Wakala wa Vipimo Mkoa wa Shinyanga, Leo Patrick, aliyabainisha hayo jana wakati wa Mkutano Mkuu kwa vyombo vya watoa huduma ya maji ngazi ya jamii, kwa lengo la kujadili, kutathimini na kubadilishana uzoefu kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu maji safi, uliofanyika Manispaa ya Kahama.

Alisema, malalamiko mengi ya ongezeko la ankara za maji kila mwezi kwa watumiaji wa huduma hiyo yanasababishwa na uvujaji wa maji katika mabomba yaliyopo chini ya ardhi ikiwa ni pamoja na dira za maji kutokaguliwa na wakala wa vipimo ili kujua kama zinafanyakazi vyema kabla ya kuzifunga kwa wateja.

Patrick alisema, ili kuondoa tatizo hilo kwa wananchi, wameanza kukagua dira za maji na kutoa elimu kwa kuanza na wateja wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Shinyanga (SHUWASA) na kuziweka alama kuonyesha zimekaguliwa na zinafaa kwa matumizi.

Alisema, baada ya kuhitimisha ukaguzi wa dira hizo SHUWASA watajielekeza katika Mamlaka ya Maji Kahama (KUWASA) na lengo ni kuondoa malalamiko ya watumiaji wa huduma ya maji ili kila mteja alipe ankara kwa anachokitumia.

Awali, akitoa taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maji, Meneja wa RUWASA, Mhandisi Maduhu Magili alisema, katika bajeti ya kipindi cha mwaka 2021/2022, walipanga kutekeleza miradi 26 katika Halmashauri za Msalala USHETU na Manispaa ya Kahama, miradi mitano ni ya ukamilishaji na 21 ni mipya.

Alisema, miradi hiyo inajumuisha pia miradi ya utafutaji wa vyanzo vipya vya maji na yote ilitengewa bajeti ya Sh. bilioni 8.842 na hadi mwezi Aprili 30, mwaka huu, fedha zilizotolewa na kutumika kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ni kiasi cha Sh. bilioni 6.685 sawa na asilimia 75.6.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Msalala, Flora Sagasaga alisema, kuna maeneo wanatumia maji na mifugo na kuiomba serikali kuelekeza nguvu katika maeneo ya vijijini ambayo yanakabiliwa na ukosefu wa huduma ya majisafi na salama.

Diwani wa Ngogwa, Kamuli Mayunga alisema, kuna mradi wa maji umekamilika kwenye kata yake, lakini haujaanza kutoa huduma kwa wananchi hali ambayo inasababisha wananchi kuendelea kushambuliwa na fisi wakati wakielekea kutafuta maji nyakati za alfajiri.

# Kampuni uwekezaji mafuta, gesi kuwezeshwa kifedha

**Na Frank Monyo**

KAMPUNI za Kitanzania zenye nia ya kushiriki katika shughuli mbalimbali kwenye miradi mikubwa ya mafuta na gesi zimehakikishiwa upatikanaji wa huduma za kifedha zitakazowezesha kushiriki vyema katika miradi hiyo.

Akiongea wakati wa tukio lililowakutanisha wanachama Jumuiya ya Watoa Huduma wa Sekta ya Mafuta na Gesi (ATOGS) Pamoja na taasisi za fedha, Mkuu wa Kitengo cha Mifumo ya Miamala wa Benki ya NMB, Linda Teggis alisema benki hiyo ipo tayari kuwasaidia Watanzania kunufaika na miradi mikubwa ya mafuta na gesi.

Alisema benki ya NMB inatambua mchango wa wazawa kwa uchumi wa nchi na kwamba tayari imeshaandaa bidhaa mbali mbali za kifedha maalum kwa ajili ya kuwawezesha wazawa kushiriki na kunufaika na miradi hiyo.

"Tunafahamu moja kati ya changamoto inazozikumba kampuni nyingi za kitanzania kushiriki katika miradi mikubwa kama hii ni upatikanaji wa mitaji. Benki ya NMB kwa kutambua hili imejipanga kuwasaidua wazawa na tunaweza kukopesha kampuni moja hadi shilingi bilioni 320," alisema.

Mwenyekiti wa ATOGS, Abdulsamad Abdulrahim alisema jumuiya hiyo inafanya kazi na wadau mbali mbali ikiwamo taasisi za fedha za lengo likiwa ni kuhakikisha wazawa wanaweza kunufaika na miradi hiyo.

"Tunayo furaha kubwa kuwa na wadau kama NMB ambao wametuhakikshia kuwa wanachama wetu watapata huduma za kifedha zitakazowawezesha kushiriki vyema katika fursa zilizopo kwenye miradi ya mafuta na gesi," alisema.

Mwenyekiti huyo alizitaka kampuni za Kitanzania kutumia fursa zilizopo na zinazokuja na zingine ambazo hazijajiunga na ATOS kufanya hivyo ili kujua kila kinachoendelea katika sekta hiyo na kuvuna faida zake.



Meneja Rasilimali Watu wa Mgodi wa Bulyanhulu, Chrispin Ngwaji, akiongea katika kongamano la kuwajengea uwezo wanafunzi wa vyuo vikuu lililoandaliwa na taasisi ya AIESEC Tanzania lililofanyika mwishoni mwa wiki katika Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU) kwa udhamini wa kampuni ya madini ya Barrick. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Makala ataka shule zitoze ada nafuu

**Na Joseph Mwendapole**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makala, amezitaka shule binafsi nchini kutoza ada nafuu, ili kusaidia Watanzania wengi kumudu kusomesha watoto wao.

Alitoa wito huo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, alipokuwa mgeni rasmi kwenye mahafali ya 14 ya kidato cha sita kwenye shule ya St. Anne Marie Academy, iliyoko Mbezi Kim ara kwa Msuguri.

"Nashauri ada ya shule iwe himilivu, shule ziweke ada ambayo haiwezi kuwashinda wazazi wenye vipato vya kati kusomesha watoto wao na hiyo itatoa fursa kwa watanzania wengi kumudu kuwalipia ada watoto wao," alisema Makala.

Katika hatua nyingine, Makala alimpongeza Mbunge wa Bukoba Vijijini (CCM), Dk. Jasson Rweikiza kwa uwekezaji mkubwa alioufanya kwenye sekta ya elimu.

Alisema uwekezaji huo umeongeza juhudi za serikali kuhakikisha Watanzania wengi wanapata elimu na kutoa ajira kwa Watanzania wengi.

"Nimeambiwa kuna walimu zaidi ya 200 hapa, walinzi, watendaji wa mazingira, makatibu muhtasi, madereva, hili ni jambo kubwa na sisi serikali lazima tumpongeze na kumtia moyo ili aendelee kutoa huduma hii muhimu kwa Watanzania," alisema.

Pia, aliwapongeza wazazi /walezi wa wanafunzi wa kidato cha sita waliohitimu kwa kutimiza wajibu wao wa kuwalea na kuwalipia ada, ili wapate elimu bora katika shule bora.

Makala pia alipongeza uongozi wa shule hiyo kwa usimamizi mzuri wa shule hali iliyosaidia kufanya vizuri katika mitihani ya kitaifa.

"Nimesikia hapa kwenye taarifa kwamba matokeo ya darasa la nne, la saba, kidato cha pili, kidato cha nne na kidato cha sita ni mazuri sana matokeo haya mazuri yanaonesha ni kwa jinsi gani shule hii imejipanga kuhakikisha wanafunzi wote wanaohitimu hapa wanapata matokeo mazuri," alisema.

Alisema kwa kuwa shule hiyo imezungukwa na jamii, inapaswa itoe misaada na ishiriki kwenye maendeleo ya jamii kama vile barabara, zahanati, shule, miundombinu ya maji, ulinzi na usafiri, ili kusaidia kudumisha uhusiano chanya kati ya shule na jamii.

Aidha, alisema serikali inatambua mchango mkubwa wa shule binafsi na kwamba itaendelea kuweka mazingira rafiki ili kupata shule nyingi ziweze kuwekeza kwenye elimu na kutoa huduma nzuri.

"Naamini mafanikio haya makubwa ya shule yanatokana na ushirikiano mzuri uliopo kati ya wafanyakazi wa shule hii, kujituma, kufanyakazi kwa bidii na uwekezaji mkubwa uliofanywa na uongozi wa shule hivyo naomba msirudi nyuma endeleeni kufanya kazi zenu kwa bidii ili shule hii iendelee kupaa siku hadi siku," alisema.

Awali, Mkurugenzi wa shule hiyo, Dk. Jasson Rweikiza, alisema ataendelea kuboresha miundombinu ya shule hiyo ili kuhakikisha inaendelea kufanya vizuri kwenye mitihani yote ya ndani na ya kitaifa.

Alisema shule hiyo itamsomesha bure mwanafunzi yeyote atakayefiwa na mzazi akiwa anaendelea na masomo shuleni hapo na kwamba wapo ambao walifiwa na wazazi na hawakurudishwa nyumbani kwa kukosa ada.

# 'Lipeni ankara miradi iwe endelevu'

**Na Restuta Damian,** KYERWA

WANANCHI wilayani Kyerwa mkoani Kagera, wametakiwa kutambua miradi ya maji inayotekelezwa na serikali inakuwa endelevu iwapo watachangia fedha zitakazosaidia kukarabati miundombinu inapoharibika au kuchakaa.

Wito huo ulitolewa hivi karibuni na Meneja Wakala wa Usambazaji Huduma ya Maji Mijini na Vijijini (RUWASA) wilayani humo, Mhandisi Shukrani Tungaraza, wakati akitoa taarifa ya upatikanaji wa maji kwa wananchi kwa kipindi cha mwezi Januari hadi Aprili, mwaka huu.

Alisema RUWASA inaendelea na ujenzi wa miradi ya maji kwa bajeti ya mwaka 2021/22 inayonufaisha wananchi zaidi ya 180,000, ambao wanatakiwa kulipa ankara za maji ili iwe endelevu.

"Miradi iliyokamilika ni saba imegharimu Sh. bilioni 1.3 kwenye maeneo yote ya miradi na wananchi wananufaika na maji," alisema Tungaraza.

Alisema katika kuhakikisha miradi hiyo inakuwa endelevu jumuiya za usimamizi wa maji kwenye vijiji na vitongoji zinakusanya fedha kama sehemu ya uchangiaji gharama za matengenezo ya miundombinu inapoharibika.

"Ziliundwa jumuiya za maji ambazo zitasimamia miundombinu ya maji kwa wananchi sambamba na ukusanyaji wa mapato yanayotolewa na watumiaji maji," alisema Tungaraza.

Aidha, alisema zipo jumuiya hazikusanyi fedha kutoka kwa wananchi kutokana na mwitiko mdogo na imani kuwa vyanzo vya maji ni mali ya wanachi na hawatakiwi kuchangia huduma hizo.

Naye, Mhasibu wa Maji Jumuiya ya Nyaruki, Donatha Benard, alisema changamoto kubwa ni mapato kidogo kutoka kwa watumiaji maji uelewa wa wananchi.

Mathalani, alisema kwa Januari hadi Aprili, mwaka huu, kwenye vijiji vinne walikusanywa Sh. 216,000 pekee. "Jumuiya ya Nyaruki kuna vijiji nne pekee ambavyo vina wananchi 30 wanaotumia maji kwa malipo zikiwa taasisi kama zahati na shule," alisema Benard.

Kadhalika, alisema miradi mingi ya maji inashindwa kulipiwa fedha iliyokubaliwa na koki za kufungulia maji zikiharibika vituo hufungiwa huduma. Mkuu wa Wilaya ya Kyerwa, Rashid Mwaimu, alisema lengo ni kusogeza huduma za maji ndani ya mita 400, na kwamba ni lazima wananchi kuchangia ili kuwa na akiba ya kukarabati miundombinu huduma iwe endelevu.

NIPASHE JUMATATU MEI 30 , 2022
Nipashe
Spotika



MAMBO MA5 ULIYOKOSA FAINALI YA LIGI YA MABINGWA ULAYA 2021/22 UK. 12-13




# WACHEZAJI WANNE WATAKAOTIKISA USAJILI

**LONDON,** England

DIRISHA la uhamisho wa majira ya joto 2022, litafunguliwa hivi karibuni na tunaweza kuona uhamisho wa hali ya juu ukifanyika katika kipindi cha miezi michache ijayo.

Katika dirisha la uhamisho wa majira ya joto la 2021, lilikuwa mojawapo ya yale ya kusisimua zaidi katika miaka ya hivi karibuni. Mikataba mingi ya hali ya juu ilivunjwa msimu uliopita wa majira ya joto. Hata nyota wakubwa wa soka, Lionel Messi na Cristiano Ronaldo, walibadili klabu huku kukiwa na shangwe kubwa.

fedha nyingi zilitumika katika dirisha la uhamisho wa majira ya joto la 2021

Jack Grealish kwenda Manchester City (euro milioni 117), Romelu Lukaku kwenda Chelsea (euro milioni 113), Jadon Sancho kwenda Manchester United (euro milioni 85) zilikuwa dili ghali zaidi. Paris Saint-Germain ilivamia soko la wakala bila malipo kusajili wachezaji kama Gianluigi Donnarumma, Sergio Ramos na Georginio Wijnaldum.

Pia walilipa euro milioni 70 kumsajili Achraf Hakimi kutoka Inter Milan. Msimu huu wa majira ya joto, klabu nyingi kubwa barani Ulaya kwa mara nyingine zinapigania kuimarisha vikosi vyao.

Hapa tunaangalia uhamisho wa wachezaji wanne mkubwa zaidi ambao unaweza kutokea katika dirisha hili la usajili wa majira ya joto.

### #4. Gabriel Jesus kwenda Arsenal

Huku Erling Haaland na Julian Alvarez wakithibitishwa kujiunga na Manchester City msimu wa majira ya joto, mshambuliaji wa Brazil, Gabriel Jesus katika klabu hiyo nafasi yake inaweza kuwa adimu. Manchester City wanatarajiwa kumtoa Jesus na kwa mujibu wa Fabrizio Romano, Arsenal wako tayari kutoa ofa ya kumnunua.

Mikataba miwili ya Lacazette na Nketiah inamalizika msimu huu wa majira ya joto na wana uwezekano wa kuondoka pale Emirates na 'Washikabunduki' hao wanahaha kutafuta mshambuliaji. Romano anadai kuwa City wanataka kiasi cha euro milioni 50 hadi 60 kwa ajili ya Jesus.

Wakala wa Jesus, Marcelo Pettinati ameripotiwa kumwambia Romano kwamba, wanapenda ajiunge na Arsenal. Jesus amefunga mabao 13 na kutoa asisti 12 katika mechi 40 kwenye mashindano yote na anaweza kuwa fiti kwa upande wa kocha Mikel Arteta. Ikiwa Arsenal iko tayari kufika bei inayotakiwa na City, dili hili linaweza kukamilika hivi karibuni.

### #3. Frenki de Jong kwenda Man United

Kuna mambo machache yanayohusika ambayo yanaashiria uwezekano wa Frenkie de Jong kusajiliwa na Manchester United msimu huu wa majira ya joto. 'Mashetani Wekundu' hao wanahitaji sana viungo wenye ubora. Kocha wa zamani wa De Jong katika klabu ya Ajax pia atainoa Man United.

Ingawa Barcelona hawana nia ya kumuuza Mholanzi huyo, wanahitaji kutafuta njia ya kupata fedha ili kuimarisha nafasi nyingine. Kutokana na matatizo yao ya kifedha, Barcelona wako tayari kukubali dili la euro milioni 60 kwa De Jong, kwa mujibu wa Goal.

Man United watakuwa na fedha kwa ajili ya uhamisho huo, lakini hawapo kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, hivyo wanaweza kushindwa kumnasa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25.

### #2. Aurelien Tchouameni kwenda Liverpool

Liverpool imekuwa moja ya timu zilizotawala zaidi barani Ulaya msimu huu. Tayari wamebeba Kombe la Carabao na la FA.

Timu hii ya Liverpool imejaa wachezaji wa kiwango cha kimataifa ambao pia wameonyesha vita na njaa nyingi. Wanaweza kuimarika zaidi msimu huu wa majira ya joto na kwa mujibu wa Ekrem Konur wa Fichajes, Liverpool wako kwenye mazungumzo na AS Monaco ili kumsajili Aurelien Tchouameni.

Kiungo huyo wa kati wa Ufaransa amekuwa mmoja wa nyota bora kwenye msimu wa Ligue 1 wa 2021-22. Anaweza kuifanya safu ya kiungo ya Liverpool kuwa bora zaidi.

AS Monaco wanaripotiwa kutaka euro milioni 55 hadi 60 kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22. Liverpool wana uwezo mkubwa katika uhamisho na halitakuwa jambo la kushangaza kama watamsajili kwa dau la chini. Hii inaweza kuwa moja ya mikataba mikubwa ya uhamisho wa majira ya joto.

### #1. Robert Lewandowski kwenda Barcelona

Baada ya mchezo wa mwisho wa msimu wa Bayern Munich dhidi ya Wolfsburg, mshambuliaji nyota, Robert Lewandowski alifichua kwamba, huenda ukawa mchezo wake wa mwisho kwa klabu hiyo. Katika mahojiano baada ya mechi, alisema (kupitia Fabrizio Romano): "Inawezekana huu ulikuwa mchezo wangu wa mwisho kwa Bayern. Siwezi kusema hivyo kwa asilimia 100, lakini inaweza kuwa (mchezo wangu wa mwisho). Tunataka kupata suluhisho bora kwangu na kwa klabu."

Kwa mujibu wa Romano, Lewandowski ana nia ya kutaka kujiunga na Barcelona. Inadaiwa zaidi kuwa Barcelona wamekubaliana maslahi binafsi na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33. Wameripotiwa kuwa tayari kumpa mkataba wa miaka mitatu ambao anautaka.

Kilichobaki kufanya sasa ni Barcelona na Bayern Munich kukubaliana kuhusu ada. Lakini kutokana na Lewandowski kushinikiza kujiunga na miamba hao wa Katalunya, Wabavaria hao huenda wakaidhinisha uhamisho huo hivi karibuni.


## ISIKUPITE

CARLO Ancelotti, amekuwa kocha wa kwanza katika historia ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kutwaa kombe hilo mara nne, lakini pia amelibeba taji hilo mara mbili katika Jiji la Paris baada ya kufanya hivyo mwaka 2007 na mwaka huu.



## Extra Time

# MAMBO MA5 ULIYOKOSA FAINALI YA LIGI YA MABINGWA ULAYA 2021/22





**PARIS,** Ufaransa

MBELE ya Uwanja wa Stade de France uliojaa jijini Paris, juzi Real Madrid ilishinda Kombe lao la 14 la Ulaya baada ya kuifunga Liverpool bao 1-0 kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka huu.

**Liverpool walianza vema mchezo huo huku Luis Diaz na Sadio Mane wakionekana kutisha mapema. Huenda 'Wekundu' hao walipata nafasi nzuri zaidi kipindi cha kwanza wakati shuti la Sadio Mane lilipookolewa na golikipa, Thibaut Courtois.**

Hata hivyo, ni Real Madrid ambao waliweka mpira wavuni kwanza. Karim Benzema alifunga dakika za lala salama za kipindi cha kwanza. Lakini VAR ilikataa bao hilo kwani alionekana kuotea.

Baada ya kipindi cha kwanza kisicho na bao, 'Los Blancos' hatimaye walichukua uongozi kupitia kwa Vinicius Junior kwenye dakika ya lala salama. Krosi ya chini kutoka kwa Federico Valverde ilimkuta na kutia mpira wavuni.

Katika mchezo wa kusisimua pale Paris, hapa kuna mambo machache ambayo mtu anaweza kuwa amekosa katika muda wa dakika 90, haya hapa...

### #1. Mabomu ya machozi kwa mashabiki wa Liverpool

Fainali ya Ligi ya Mabingwa kati ya Liverpool na Real Madrid juzi, ilicheleweshwa kwa dakika 36. Kwa mujibu wa gazeti la The Athletic, mashabiki wa Wekundu hao waliokuwa na tiketi hawakuweza kuingia uwanjani licha ya kupanga foleni nje kwa zaidi ya saa mbili.

Ofisa Habari wa timu ya Wanawake ya Liverpool na akademi ya timu hiyo, Andy Kelly, aliripoti kwamba mashabiki walizuiwa kwa mabomu ya machozi nje ya uwanja. Kelly 'alitweet' yafuatayo kabla ya kuanza kwa mchezo huo:

"Mashabiki wakiwa wamepanga foleni nje wakiwa na tiketi za kuingia kwenye geti ambalo limefungwa bila sababu kwa kupigwa mabomu ya machozi. Kupitia uzoefu mbaya na hatari sana. Hivi sivyo mashabiki wanapaswa kutendewa katika jamii iliyostaarabika. Haikubaliki."

Mchezo huo ulicheleweshwa kwa dakika 15. Hata hivyo, ucheleweshwaji huo uliongezwa baadaye ambapo uliwalazimu pande zote mbili kutoka nje ya uwanja kwa raundi ya pili ya maandalizi ya mchezo kabla ya mchezo. Wakati wa mchezo huo, Wekundu hao walitoa taarifa rasmi wakiomba uchunguzi rasmi kuhusu masuala ya kabla ya mechi na mashabiki.

### #2. Nyota wa Tenisi, Rafael Nadal ashangiliwa na mashabiki wa Real Madrid

Nyota wa Tenisi, Rafael Nadal alishangiliwa na mashabiki wa Real Madrid wakati Mhispania huyo alipoonyeshwa kwenye skrini kubwa kabla ya mchezo kuanza. Nadal ni shabiki mkubwa wa 'Los Blancos' hao na alikuja hapo Stade de France kutoa msaada wake kwa upande wa LaLiga.

Nadal kwa sasa yuko Paris akishiriki mashindano ya 2022 Roland Garros (French Open). Mhispania huyo mwenye umri wa miaka 35, anakodolea macho taji lake la 14 la French Open wakati huu.

Nadal jana Jumapili alitarajiwa kumenyana na Mkanada Felix Auger-Aliassime katika Raundi ya 16-Bora ya French Open. Hata hivyo, hilo halikumzuia kuwaunga mkono Real Madrid katika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Liverpool.

### #3. Upinzani wa Ibrahima Konate kwa Vinicius

Mashabiki wa Liverpool walikuwa na wasiwasi kidogo baada ya kuona jina la Ibrahima Konate kwenye kikosi cha kwanza badala ya Joel Matip. Hata hivyo, wasiwasi huo uliondolewa haraka baada ya kuweza kumdhibiti vilivyo winga wa Real Madrid, Vinicius Junior.

Kinda huyo wa Brazil alikuwa akitafuta kutengeneza kitu kwenye upande wa kulia wa safu ya ulinzi ya Liverpool. Vinicius alijaribu kuuwahi mpira kwenye eneo la hatari, lakini mbio zake zilizuiwa na Konate na baadaye akazidiwa misuli na Mfaransa huyo.

Konate aliwasili Anfield msimu uliopita wa majira ya joto akitokea RB Leipzig ya Bundesliga. Beki huyo mwenye umri wa miaka 23, alicheza mechi 28 kwa Wekundu hao kabla ya fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

### #4. Virgil van Dijk alicheza kama mshambuliaji

Liverpool katika dakika za lala salama, Jurgen Klopp alimwagiza mlinzi Virgil van Dijk kucheza kama mchezaji wa mbele. Hii ni licha ya Wekundu hao kuwa na Mohamed Salah, Diogo Jota, Roberto Firmino na Sadio Mane uwanjani.

Dijk alionekana kuwa tishio kutokana na uchezaji wake na kimo chake cha urefu.

### #5. Raul alimfariji Klopp

Mshambulizi wa zamani wa Real Madrid, Raul alimfariji kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp wakati yeye na timu yake wakiwatazama wapinzani wao wakinyanyua taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya. Kikosi kizima cha Liverpool kiliwangoja Los Blancos uwanjani kunyanyua kombe hilo kabla ya kuwapigia makofi wapinzani wao.

Klopp na wachezaji wake walisimama pamoja kutazama Real wakinyanyua kombe kabla ya kuondoka. Raul aliamua kwenda kumfariji Klopp wakati wakiondoka.

Wekundu hao sasa wamepoteza fainali yao ya pili ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Real Madrid katika miaka ya hivi karibuni.

## Nukuu

"Mechi ngumu zaidi kwenye Ligi ya Mabingwa msimu huu? Mechi dhidi ya Chelsea pale [Uwanja] wa Bernabeu. Ilikuwa ngumu sana kiakili kwa sababu tulishinda London," **Kocha wa Real Madrid, Carlo Ancelotti. Katika mechi hiyo Madrid walishinda 3-1 wakiwa Stamford Bridge na mchezo wa marudiano nyumbani hadi dakika ya 79 Chelsea ikawa inaongoza 3-0 kabla ya wenyeji hao kupata mabao mawili dakika ya 80 na 96 na kusonga mbele kwa mabao 5-3.**



"Ten Hag atataka Rangnick aondoke tu. Ningekuwa Ten Hag ningemwambia Rangnick aondoke zake na kusema 'nitafanya hivi mwenyewe. Hujafanya chochote tangu umekuja, nataka nianze upya na watu wangu. Sidhani kama anamhitaji Rangnick pale hata kidogo. Haiingii akilini kwake kuwa bado pale pamoja na yeye kuchukua kazi kuinoa Austria. Anapaswa kuwa ameondoka," **mshambuliaji wa zamani wa Aston Villa, Gabriel Agbonlahor anaamini kuwa kocha mpya wa Manchester United, Erik ten Hag , hapaswi kuwa na Ralf Rangnick.**



"Naamini nilikuwa namba moja, najiweka namba moja moja kwa moja ndivyo ninavyokabiliana na kila kitu. Namba mbili nitaenda kwa Vidic, mpenzi katika uhalifu, nadhani aliongoza kwa mfano, hajawahi. sema sana.'mimi nilikuwa mzungumzaji, mpangaji, alikuwa mnyama. Ni mchezaji pekee niliyemuona washambuliaji walimtazama na kuwaza 'Woah', tazama pua yake, alitumia kichwa kupitia watu kushinda mpira lakini kwa kweli alikuwa mwanasoka bora kuliko watu wanavyofikiria, alisoma mchezo vizuri sana, tulikuwa na ushirikiano mzuri," **beki wa zamani wa Manchester United, Rio Ferdinand akidai kwamba yeye na Nemanja Vidic ndio mabeki wawili bora katika historia ya Ligi Kuu England.**



Nipashe
Spotika



Mfungaji wa bao pekee dhidi ya Simba juzi katika Uwanja wa CCM Kirumba, Kiungo wa Yanga, Salum Abdallah 'Fei Toto' **PICHA: MAKTABA**

# YANGA KICHEKO, SIMBA NA 'MWAKA WA SHETANI'

**Na Adam Fungamwango**

ILIKUWA ni moja kati ya mechi chache za watani wa jadi ambazo huwa zinachezwa nje ya Jiji la Dar es Salaam. Uwanja wa CCM Kirumba juzi kuanzia saa 9:30 Alasiri ulizipokea timu kongwe na zenye mashabiki wengi nchini, mechi iliyomalizika kwa Yanga kushinda bao 1-0.

**Lilikuwa ni bao la juhudi binafsi za kiungo Feisal Salum 'Fei Toto' kuachia fataki kali umbali wa mita 35, lililokwenda moja kwa moja wavuni na kumuacha kipa Beno Kakolanya akiruka baada ya mpira kujaa wavuni.**

Baada ya bao hilo, timu hizo zilicheza kwa dakika 65 zilizobaki bila mafanikio na hadi mwamuzi Ahmed Aragija alipopuliza kipenga cha kumaliza mechi hiyo, Yanga ikawa imetinga hatua ya fainali ya Kombe la FA, na kuivua rasmi ubingwa huo Simba.

Ikawa pia imehitimisha msimu mbaya kwa 'Wekundu wa Msimbazi' kwani pia haina uhakika kabisa wa kutwaa ubingwa wa Tanzania Bara msimu huu. Ilichofanikiwa kuchukua ni Kombe la Mapinduzi ililolipata mwanzoni mwa mwaka huu kwa kuifunga Azam FC bao 1-0 kwenye Uwanja wa Amaan, Zanzibar.

**Yanga yalipa kisasi**

Ni ushindi ambao umeifanya Yanga kulipa kisasi cha kufungwa mechi ya fainali ya kombe hilo msimu uliopita kwenye Uwanja wa Tanganyika, Kigoma Julai 25, mwaka jana, Simba ikishinda 1-0 kwa bao la Thadeo Lwanga.

Yanga pia imelipa kisasi cha kufungwa mechi ya nusu fainali ya michuano hiyo misimu miwili iliyopita kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, iliponyukwa mabao 4-1, Julai 12, 2020, yakifungwa na Gerson Fraga, Clatous Chama, Luis Miquissone na Mzamiru Yassin.

Kati ya wafungaji hao ni wawili tu waliosalia kwenye kikosi hicho ambao ni Chama ambaye hata hivyo hakucheza kwenye mechi hiyo kutokana na kuwa majeruhi, huku Mzamiru pekee ndiye aliyecheza. Aliyefunga bao la kufutia machozi ni Fei Toto, naye ndiye aliyepeleka kilio Mzimbazi juzi.

**Ngao ya Jamii, Ligi hadi FA**

Ni msimu ambao Yanga imekuwa mbabe kwa Simba, baada ya kushinda mara mbili kwenye michuano mingine, huku Wekundu wa Msimbazi wakifanikiwa kulazimisha suluhu kwenye mechi zote za Ligi Kuu.

Ulionekana mapema ni mwaka wa kicheko kwa Yanga na wa shetani kwa Simba, kwenye mechi ya Ngao ya Jamii Septemba 25, mwaka jana, Yanga ilishinda bao 1-0, lililofungwa na Fiston Mayele.

Zilikutana mara ya kwanza mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Desemba 11, mwaka jana na kutoka suluhu bila kufungana, lakini matokeo kama hayo yalipatikana zilipocheza mechi ya mzunguko wa pili Aprili 30, mwaka huu.

Ilionekana kama tayari wameshamalizana msimu huu, lakini baada ya kila mmoja kushinda kwenye FA, droo ikapangwa, ikabidi zikutane na hapo ilikuwa ni lazima apatikane mbabe na Yanga ikadhihirisha kuwa msimu huu haitanii kwa ushindi mwingine wa bao 1-0 juzi.

**Timu ziligawana vipindi**

Kwenye mechi hiyo, Yanga ilitawala zaidi kipindi cha kwanza na Simba ikauchukua mchezo kipindi cha pili.

Hata hivyo, ni Yanga ambao walifanya mashambulizi mengi ya hatari kipindi ambacho walitawala, tofauti na kipindi ambacho Simba waliutawala mchezo.

Shambulizi la hatari zaidi kwa Simba kipindi cha kwanza lilikuwa dakika ya 37, Chris Mugalu alipounganisha kwa kichwa mpira wa faulo ya Mohamed Hussein 'Tshabalala', lakini kipa wa Yanga, Djigui Diarra alijinyoosha upande wake wa kushoto na kwenda kudaka mpira.

Ni kipindi ambacho Yanga ingekuwa makini ingekuwa na mabao manne, kwani pamoja na kupata bao moja, ilifanya mashambulizi hatari matatu ya yote yalimhusisha Mayele.

Mayele tena 'alimkamua' Joash Onyango, akaingia hadi hatua tatu tu kutoka golini, lakini aliamua kuwa mchoyo kwa kutaka kufunga mwenyewe, shuti lake hafifu likambabatiza Kakolanya na kuzagaa eneo la hatari, kabla hajauwahi na kuudaka.

Dakika ya 90 ndipo Simba ilifanya shambulizi hatari kwa mpira wa kona ya Rally Bwalya na kupigwa kichwa na Onyango, ukagonga mwamba wa juu na kurejea uwanjani, ukamkuta Mhilu ambaye uliurudisha golini, lakini ukawababatiza mabeki wa Yanga na kurejea uwanjani.

**Wachezaji wa Simba hawana nguvu**

Kitu kilichoonekana kwenye mechi hiyo ni kwamba wachezaji wengi wa Simba walionekana wavivu kupambana.

Wakati wao walipasiwa mpira, wachezaji wa Yanga waliwafuata kwa nguvu ili kuwanyang'anya au kuwatia presha, lakini walikuwa wakiwaachia kwanza wachukue mpira na baada ya hapo ndiyo wawafuate, kitu ambacho kiliwafanya wawe watumwa uwanjani.

Pia walishindwa vita' ya kunyang'anya mpira moja kwa moja dhidi ya mchezaji wa Yanga wanapogombania.

Wachezaji wa Yanga walionekana kuwa na nguvu na wakakamavu dhidi ya Simba, ambao hata wakiwa wawili walishindwa kuuchukua mpira dhidi ya mchezaji mmoja wa Yanga, hasa pale katikati. Na hilo ni tatizo kubwa la timu hiyo msimu huu.

**Mfumo wa Nabi, Pablo**

Kilichoshangaza wengi ni kwamba Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi hakuchezesha winga hata mmoja kipindi cha kwanza, mpaka kipindi cha pili alipoingia Farid Mussa.

Badala yake alijaza viungo Yannick Bangala, Abobakar Salum, Khalid Aucho na Fei Toto. Kati ya hao, watatu, ukimuondoa Bangala, pamoja na sifa ya kuzuia, lakini pia wana sifa ya kushambulia, hiyo iliwasaidia zaidi Yanga ambao kwa kujua aina ya uwanja wa CCM Kirumba, walichezesha mastraika wawili, Hetirier Makambo na Mayele.

Kocha wa Simba, Pablo Franco yeye alikuwa na viungo watatu, Thadeo Lwanga, Sadio Kanoute na Mzamiru Yasssin ambao wote asili yao ni kuzuia zaidi kuliko kushambulia, na ndiyo maana baada ya kuingia Bwalya, timu ilichangamka na kushambulia zaidi. Aliweka straika mmoja tu Chris Mugalu ambaye hakuonekana kama anaweza kuleta hatari yoyote ile.

Kwenye upande wa ushambuliaji, Kibu Denis, aliyecheza winga ya kushoto, ndiye mchezaji pekee aliyeonekana ni hatari kwa Yanga kila anapokuwa na mpira, tofauti na Mugalu ambaye muda wote alionekana kupotea mpira akiwa amelipa mgongo lango la timu pinzani, kitu kilichowapa urahisi sana mabeki wa kati wa Yanga, Dickson Job na Bakari Mwamnyeto.

**JE, WAJUA?**



Real Madrid wamekuwa wakiishi kwa ngozi ya meno linapokuja suala la Ligi ya Mabingwa Ulaya, na msimu huu imeonyesha ukubwa wake kwani hadi inatwaa taji hilo juzi, imezipiga Paris St- Germain, Chelsea, Manchester City na Liverpool.



## HABARI DODOMA

# DC aonya wanaovamia maeneo ya uwekezaji

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, ameonya wananchi kuacha kuvamia maeneo ya umma yaliyotengwa kwa uwekezaji wa miundombinu mbalimbali.

Shekimweri alitoa onyo hilo jana kwenye ziara yake ya kutembelea miradi ikiwamo eneo la uwanja wa ndege wa kimataifa utakaojengwa Msalato na Shule ya Sekondari ya Hombolo Makulu.

Onyo hilo lilitokana na mkazi mmoja wa Kata ya Hombolo Makulu, kujenga nyumba ndani ya eneo la shule ya sekondari na hivyo kuagizwa kuibomoa.

Alisema kuwa maeneo hayo yametengwa kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kiserikali,hivyo hakuna sababu ya watu kuanza kuvamia na kujenga majengo.

Aliwataka wananchi kujiepusha na tabia hiyo ya kuvamia maeneo ambayo yameshatengwa kwa ajili ya miundombinu ya umma.

Aidha, aliwataka wananchi wa kata hiyo kuwa na mwamko wa kuwekeza kwenye elimu ili watoto wao wafikie ndoto zao kielimu.

Kwa upande wake, Ofisa Elimu Sekondari wa Jiji la Dodoma, Upendo Rweyemamu, alisema kuwa kuwapo kwa shule hiyo kutasaidia watoto kuondokana na kero ya kutembea kwa umbali mrefu kufuata shule.




Mkurugenzi Mkuu Kampuni ya Mafuta ya TotalEnergies, Jean Francois Schoepp (kulia) akikata utepe kuzindua kituo cha cha mafuta cha TotalEnergy eneo la Mapinga, Bagamoyo mkoani Pwani, kinachomilikiwa na Mtanzania, kwa utaratibu uitwao DODO. Kushoto ni Mmiliki wa Kituo hicho Jakson Swai, katikati ni Joyce Swai (Mke wa mmiliki). Hiki ni kituo cha 14 cha TotalEnergy kinachoendeshwa kwa mpango wa DODO, ambao ni Mtanzania kujengewa uwezo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bashungwa ahimiza uwajibikaji utumishi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Innocent Bashungwa, amewataka maofisa utumishi kuwa waadilifu, wabunifu na wenye kuwajibikaji kwa hiari ili kutoa huduma bora kwa wananchi.

Bashungwa aliyasema hayo juzi jijini hapa alipokuwa akifunga kikao kazi cha Wakuu wa Idara na Vitengo vya Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma.

"Nyie ni mameneja wa rasilimaliwatu, sasa unampimaje mtumishi ni kulingana na anachopata na anachozalisha, na shughuli yetu kubwa kwa serikali ni kutoa huduma bora kwa wananchi, naomba mkazingatie," alisema.

Aidha, Bashungwa aliagiza maofisa hao waliopo kwenye Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwasaidia Wakurugenzi kwenye kufanya maamuzi ya kiutendaji katika halmashauri zao.

"Ninyi mna mamlaka ya kumshauri Mkurugenzi kufanya maamuzi sahihi ya kiutumishi timizeni wajibu huo kwa kutenda haki, pamoja na kusimamia maadili ya utumishi wa umma."

"Pia, mna wajibu wa kusimamia miradi ya maendeleo kwa sababu inatekelezwa na watumishi, tukifuatilia utendaji kazi katika maeneo yenu na kukuta changamoto, Ofisa Utumishi utawajibika sababu unakuwa umeshindwa kusimamia kazi yako ya rasilimaliwatu," alisisitiza.

Waziri Bashungwa alitoa maelekezo kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Utumishi, Dk. Laurean Ndumbaro kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kufanyia kazi suala la Maofisa Utumishi wanaokaimu nafasi hizo kwa muda mrefu.

Naye, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi, aliwataka maofisa hao kutunza siri za serikali na kupima ubora wa utendaji kazi wa watumishi.

"Watumishi wa umma tuna deni kubwa kwa Rais wetu Samia tayari yeye ameonesha kwa vitendo kuwajali watumishi na ameongeza mishahara lakini ametoa kibali cha kuongeza posho kwa watumishi, tumlipe Rais wetu kwa kufanya kazi kwa bidii," alisema.

Mwenyekiti wa Maofisa Utumishi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, Tabia Mohamed, alisema kikao hicho kimesaidia kuwakumbusha majukumu yao pia kujifunza utumiaji wa mfumo mpya wa kuweka taarifa za watumishi ikiwamo mfumo wa usimamizi wa utendaji kazi kwa watumishi wa umma (PEPMIS).

# Watafiti watakiwa kufuata takwimu sehemu sahihi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imewataka wadau wanaotaka kufanya tafiti katika masuala ya afya kwenda kutafuta takwimu sehemu sahihi kwa ajili ya kufanya utafiti badala ya kutoa malalamiko ya kuwa hawapewi ushirikiano.

Mkurugenzi wa Huduma za Afya, Ustawi Jamii na Lishe, kutoka Ofisi ya Rais, Serikali za Mitaa na Tawala za Mikoa (TAMISEMI), Dk. Ntuli Kapologwe, aliyasema hayo wakati wa mdahalo wa kujadili masuala ya ubunifu katika sekta ya afya.

Dk. Kapologwe alisema wamebaini kuwa wengi wa wanaotaka kufanya utafiti wanachelewa kufanya utafiti wao kwa kuomba takwimu kwa ajili ya muongozo wa ufanyaji utafiti kwenye sehemu ambazo hazistahili kufanya hivyo.

"Serikali inapenda kuona tafiti mbalimbali na bunifu zinafanyika, kwa sababu zinasaidia kubuni vitu ambavyo vinaleta afua kwa serikali ikiwamo kutatua changamoto mbalimbali," alisema.

Alisema takwimu katika Wizara ya Afya zinahitaji umakini kwa sababu zikitolewa ovyo zinaweza kuleta madhara kwa watoa taarifa hiyo pamoja na jamii ambao ni walengwa wa utafiti unaotaka kufanyika.

"Mkihitaji takwimu kwa upande wa Afya mnatakiwa kwenda Wizara ya Afya na TAMISEMI na si kwingineko mnapaswa kulitambua hilo," alisema Dk. Kapologwe.

Alisema wanaunga mkono jitihada za wadau mbalimbali, sekta binafsi, vyuo na wengineo ambao wanasaidia serikali kuleta ubunifu ili kuboresha utoaji huduma katika sekta ya afya.

Mkurugenzi huyo alisema kwa kipindi cha miaka miwili hadi mitatu, serikali imepokea bunifu mbalimbali zikiwamo za usimamizi wa fedha kwenye ngazi ya vituo vya kutolea huduma na ngazi ya msingi na za kukabiliana na watoto wenye tatizo la upumuaji.

Alisema serikali itaendelea kushirikiana nao ili kuhakikisha kwamba inatengeneza mazingira wezeshi kwa wabunifu kutoka ngazi ya jamii, vituo vya afya, rufani mkoa hadi taifa. Alipongeza kampuni ya Vodacom kwa kuwezesha wabunifu kwa upande wa vijana hususani wa kike katika kujiendeleza kupitia bunifu zao. Naye, Mkurugenzi wa Huduma za Kidigital kutoka Vodacom Tanzania, Nguvu Kamando, alisema tangu programu ya Digital Accelerator ianze imesaidia zaidi ya kampuni 15 za wajasiriamali ambapo kati ya hizo nne tayari zinafanya vizuri kimataifa.

Kamando alisema Vodacom Digital Accelerator ina lengo la kuwaangalia wajasirimali wa Kitanzania kwenda kwenye ndoto zao kwa muda mfupi zaidi.





## Waiangukia serikali kuingilia kati 'lumbesa'

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

WAKULIMA wa Mpunga katika Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, wameiomba Serikali kuwadhibiti wanunuzi wa zao hilo wanaotumia vipimo visivyoruhusiwa ikiwemo ujazo mkubwa ujulikanao kama 'Lumbesa'.

Wakulima hao wameiomba serikali kuwalazimisha wanunuzi wote wa zao hilo kununua kwa kutumia mizani badala ya kupima kwenye madebe na mifuko yenye ujazo usiojulikana ili kuepuka unyonyaji unaowasababishia hasara.

Ombi hilo lilitolewa wakati wa utoaji wa elimu ya kilimo bora cha mpunga iliyotolewa na Kampuni ya usambazaji wa mbolea ya YARA Tanzania kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI), kituo cha Uyole.

Elimu hiyo ilitolewa katika shamba darasa lililoandaliwa na taasisi hizo katika Skimu ya Umwagiliaji ya Matebete iliyopo katika Kata ya Chimala, wilayani humo na wakulima hao walisema wamekuwa wakipata hasara. Mmoja wa wakulima hao, Edward Mwakifwamba, alisema baadhi ya wakulima hao, wamekuwa wakinunua mazao hayo kwa kushindilia kwenye mifuko ambayo ujazo wake haujulikani.

Alisema kitendo hicho kimekuwa kikiwasababishia hasara wakulima kutokana na kupata kipato kisichoendana na gharama za uzalishaji wa zao hilo.

"Tunataka tusaidiwe kuuza mazao yetu kwa kutumia mizani, sisi hata tukiuza kilo moja kwa Sh. 1,000 tunaamini tutapata faida nzuri na tutapata tija kwenye zao hili, lakini sio sasa hivi ambapo wanunuzi wanakuja na mifuko yao," alisema Mwakifwamba.

Akiwa ziarani mkoani Mbeya mwaka juzi, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alipiga marufuku wanunuzi wa mazao ya wakulima kutumia ujazo wa lumbesa huku akiwataka viongozi wa serikali kusimamia utekelezaji wa katazo hilo.

# Serikali yawatangazia kiama viongozi AMCOS

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

SERIKALI mkoani Mbeya imewatangazia kiama wakulima, viongozi wa Serikali na vyama vya Msingi vya wakulima wa tumbaku (AMCOS) watakaobainika kutorosha tumbaku katika Wilaya ya Chunya mkoani humo kuwa watachukuliwa hatua kali za kisheria.

Aidha imepiga marufuku kampuni za ununuzi wa tumbaku kubeba mazao ya wakulima na kuyasafirisha kabla hawajawalipa fedha zao kwa maelezo kuwa utaratibu huo unasababisha wakulima kudhulumiwa.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera alitoa tahadhari hiyo mwishoni mwa wiki alipokuwa anazindua msimu mpya wa ununuzi wa Tumbaku wilayani Chunya katika Kata ya Kambikatoto.

Homera alisema mbali na kupelekwa mahakamani pia serikali itataifisha tumbaku itakayokamatwa ikitoroshwa pamoja na vyombo vya usafiri vitakavyokamatwa vikitumika kwenye utoroshaji huo ili kufidia hasara ambayo imekuwa ikipatikana. Alisema katika miaka ya karibuni tatizo la utoroshaji wa tumbaku limekuwa likiongezeka katika Wilaya ya Chunya jambo ambalo linaikoseha Serikali mapato pamoja na kuvisababishia hasara vyama vya Msingi kutokana na tumbaku hiyo kuzalishwa kwa pembejeo za mkopo.

Aliwaagiza maofisa watendaji wa vijiji na Kata wilayani humo kushirikiana na maaskari Kata kudhibiti utoroshaji wa tumbaku na kwamba kwa wale ambao tumbaku itatoroshwa katika maeneo yao pia watashughulikiwa.

"Viongozi wa Kata zote za Tarafa ya Kipembawe ni lazima muwe makini, mmekopa zaidi ya Sh. Bilioni saba, sasa tumbaku ikitoroshwa mtarejesha mkopo huo na nini? Sasa ikitokea tumbaku ikatoroshwa kwenye eneo lako ujuwe na wewe uko matatani," alisema Homera.

Katika hatua nyingine Homera alisema kampuni zitakazowadhulumu wakulima fedha zao zitachukuliwa hatua.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon, alisema katika msimu uliopita walikamata baadhi ya wakulima wakitorosha tumbaku na wakaitaifisha tumbaku hiyo na kuwafikisha mahakamani wahusika.

Alisema mwaka huu wanakusudia kuongeza udhibiti kwenye maeneo mbalimbali ili watoroshaji wasiwapo na akawataka wakulima kuacha tabia hiyo akisisitiza kuwa watafilisiwa. Akitoa taarifa ya uzalishaji wa tumbaku wilayani humo, Kaimu Meneja wa Chama Kikuu cha Ushirika wa wakulima wa tumbaku wilayani Chunya (CHUTCU), Juma Nshishi alisema mwaka huu mavuno yameshuka kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

Alisema makisio ya uzalishaji ilikuwa Kilo 9,000,000 lakini wamezalisha Kilo 8,000,000 na kwamba tatizo kubwa ilikuwa ni mvua kuchelewa kuanza kunyesha na kuisha mapema hali ambayo ilisababisha wakulima kushindwa kuendana na msimu.

Hata hivyo alisema msimu ujao wanakusudia kuongeza uzalishaji kutokana na kuongezeka kwa kampuni nyingine ya ununuzi hali ambayo alisema itasababisha ongezeko la mahitaji.

"Vilevile tunatarajia kuongeza usajili wa wakulima kwenye vyama vya Msingi tulivyonavyo ili kuongeza uzalishaji, tunakusudia kufikia uzalishaji wa zaidi ya kilogramu 10,000,000," alisema Nshishi.

Hata hivyo baadhi ya wakulima waliwalalamikia viongozi wa vyama vyao kuwa katika msimu huu waliwanunulia baadhi ya pembejeo ambazo zilikuwa feki na hivyo kuwasababishia ongezeko la gharama za uzalishaji.



Wakulima wa vitunguu katika Skimu ya Umwagiliaji ya Igomelo katika Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, wakipalilia mazao yao mwishoni mwa wiki, eneo hilo ni miongoni mwa maeneo yanayozalisha vitunguu kwa wingi katika Mkoa wa Mbeya. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

# Waonywa kutumia uzazi wa mpango bila ushauri

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WASICHANA wameshauriwa kuepuka kutumia njia za uzazi wa mpango bila kupata ushauri wa wataalamu wa afya ili kuepuka kupata madhara ya afya ya uzazi tatizo ambalo linadaiwa kuwa linaongezeka kwa kasi katika jamii.

Aidha wametakiwa kuepuka kuanza kushiriki ngono katika umri mdogo ili kutopata mimba za utotoni pamoja na magonjwa ya zinaa ambayo yanadaiwa kuwa matatizo yanayoathiri afya ya uzazi kwa vijana hasa wasichana.

Ushauri huo ulitolewa na wataalamu wa afya wa Jiji la Mbeya wakati wa mafunzo maalumu ya kuwajengea uwezo waandishi wa habari wa Mkoa wa huo kuhusu masuala ya afya ya uzazi mafunzo yaliyoandaliwa kwa ushirikiano kati ya Timu ya Afya ya Mkoa na Shirika lisilokuwa la kiserikali la JHPIEGO kupitia mradi wake wa 'Tupange Pamoja' (TCI).

Mmoja wa wataalamu hao, Celina Kayange ambaye ni muuguzi, alisema zipo njia mbalimbali za uzazi wa mpango ambazo zimethibitishwa na Shirika la afya duniani kuwa ziko salama kwa kupanga uzazi lakini zinatakiwa kutolewa kwa utaratibu maalumu.

Alisema baadhi ya wasichana wamekuwa wakitumia dawa hizo hasa vidonge vya P2 bila kupata maelekezo ya wataalamu hali ambayo alisema ni hatari kwa afya zao za uzazi.

"Tunachosisitiza sasa hivi ni vijana kuacha kushiriki ngono katika umri mdogo, vitendo hivi ni hatari kwa afya zao lakini baadhi yao pia wanatumia dawa za uzazi wa mpango bila kupata maelekezo ya wataalamu," alisema Celina.

Mkuu wa Dawati la Jinsia na Watoto wa Mkoa wa Mbeya, Inspekta Loveness Mtemi, alisema katika mkoa huo vitendo vya ukatili wa kijinsia hasa ukatili wa kingono vimekuwa vikiongezeka kwa kasi katika mkoa huo na hivyo kuathiri afya ya uzazi kwa vijana.

Alisema kesi nyingi za ukatili wa kijinsia ambazo wamekuwa wakipokea katika dawati hilo zimekuwa zikihusu ukatili wa kingono hasa ulawiti na unajisi wa watoto na hivyo akawataka wazazi na walezi kuwa makini na watoto wao.

Alisema baadhi ya vitendo hivyo huwa vinachochewa na wazazi kuwaruhusu watoto wao kutumia simu za mkononi na kompyuta kuingia kwenye mitandao ya kijamii pamoja na kuangalia kwenye runinga bila uangalizi.

"Nawaomba wazazi msiwe mnawaacha watoto wanatumia simu zenu na kuangalia runinga muda mwingi, wanajifunza vitendo ambavyo hawastahili kujifunza, wanunulieni vitabu vitawasaidia," alisema Ins. Loveness.

Hata hivyo, alisema baadhi ya wazazi na walezi wamekuwa wakiharibu ushahidi wa kesi za unyanyasaji wa kingono kwa watoto wao kutokana na kuelewana wenyewe kwa wenyewe na hivyo kuharibu kesi.

Vilevile, aliwataka wazazi kuepuka kuwalaza watoto wao na wageni wa kiume hata kama ni ndugu kwa maelezo kuwa vitendo vingi vya ubakaji wa watoto vinafanywa na ndugu huku akisisitiza kuwa watoto wa kiume kwa sasa wana hali mbaya zaidi.

Akifungua mafunzo hayo, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Salum Manyatta, aliwataka waandishi wa habari kutumia kalamu zao kuelimisha jamii kuhusu afya ya uzazi pamoja na kuibua vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Alisema vijana wenye umri kati ya miaka 15 mapaka 24 wako katika hatari zaidi ya kupata matatizo ya afya ya uzazi ikiwa ni pamoja na kupata maambukizi ya Virusi vya UKIMWI na mimba za utotoni.



# Kesi baba anayedaiwa kumwingilia mwanawe kinyume yaendelea kortini

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAHAKAMA ya Mkoa wa Vuga, imeendelea kusikiliza kesi inayomkabili mshtakiwa Kheri Mkombe Abdallah, anayedaiwa kumwingilia kinyume na maumbile mtoto wake wa kike mwenye umri wa miaka 11.

Kesi hiyo inasikilizwa na Hakimu Omar Mcha huku upande wa mashtaka ukiwakilishwa na mawakili wa serikali Khamis Othman, Kudra Khamis na Mariyam Abdlah na upande wa utetezi ukiwakilishwa na wakili wa kujitegemea, Rajab Abdallah.

Mshtakiwa anadaiwa kutenda kosa hilo Mei 10, mwaka huu nyumbani kwake Pangawe, Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Akitoa ushahidi mahakamani, mama wa mtoto huyo (jina linahifadhiwa) ambaye ni mke wa mshtakiwa alidai kuwa majira ya saa nne usiku wa Mei 10, alimkuta mshtakiwa amekaa sebuleni akiwa hana nguo huku akiwa amempakata mtoto wake.

Alidai mbele ya mahakama hiyo kuwa hakuamini alichokiona baada ya kuona uume wa mume wake ukitoka sehemu za siri za mtoto wake.

"Ilikua majira ya saa nne usiku siku hiyo mume wangu alichelewa kurudi kazini, alipoingia nyumbani alinikuta nipo chumbani kwangu nishapanda kitandani kwa ajili ya kujitayarisha kulala na watoto wangu nimewaacha sebuleni na dada wa kazi."

Alidai baada ya mume wake kuingia chumbani alimuamsha, lakini alijifanya amelala na kutoka sebuleni akiwa amejifunga kanga ya kiuno.

Kitendo cha kutoka chumbani akiwa amejifunga kanga ya kiuno kilimfanya adhani kuwa anaenda bafuni kuoga, lakini baada ya kuona amechukua muda mrefu bila ya kurejea alikwenda kumuangalia na kumkuta sebuleni akiwa anamfanyia kitendo cha udhalilishaji mtoto wake.

"Baada ya kumfuma nikapiga kelele, akainuka ghafla na kuanza kuniziba mdomo ili nisipige kelele zaidi na kuniingiza chumbani kwangu na kuufunga mlango kwa ndani huku akiniomba radhi kuwa nimsamehe kwa kitendo alichofanya," alidai shahidi huyo.

Alidai mahakamani hapo hapo kuwa muda huo alishindwa kutoka nje kuomba msaada kutokana na mume wake kufunga mlango na ufunguo kuushikilia huku akiendelea kumtuliza na kumuomba radhi na kumuahidi atampa kitu chochote cha thamani endapo atamfichia uovu huo.

Shahidi huyo aliadi kuwa baada ya kupambazuka Mei 11, alitoka nyumbani kwenda kwa mama yake kumueleza tukio hilo na ndipo walipochukua hatua kwa kumpeleka mtoto kituo cha polisi na hospitali na daktari athibitisha alikuwa ameingiliwa.

Alidai wakati wakiendelea na hatua hizo mshtakiwa alishatoroka kusikojulikana.

Baada ya mahakama kusikiliza ushahidi wa mama, pia ilisikiliza ushahidi wa mtoto aliyedhalilishwa na kesi hiyo kuahirishwa hadi Juni 13, mwaka huu.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar akimshuhudia mwanafunzi Mudrik Salum akiweka alama ya kumbumbu skuli hapo ya kuwa mwanafunzi bora wa mwaka kutoka Shule ya Feza Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# SMZ kuendelea kuthamini shule binafsi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema kuwa itaendelea kuthamini mchango wa shule binafsi katika kuhakikisha vijana wanapata elimu bora ambayo itazalisha wataalamu wa kulisimamia Taifa. Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, aliyasema hayo katika mahafali ya sita ya wanafunzi wa kidato cha sita ya Shule ya Feza Zanzibar, yaliyofanyika katika shule hiyo Kisauni.

Alisema Sera ya Elimu ya mwaka 2006, inaeleza kuthamini sekta binafsi katika kutoa elimu na mategemeo ya serikali kupata wataalamu mbalimbali kupitia shule za serikali na binafsi.

Hemed aliupongeza uongozi wa Shule ya Feza kuwa ni mfano kwa kujitolea katika kuwafunza watoto na kuibua vipaji walivyokuwa navyo na kuwahakikishia serikali itaendelea kuthamini juhudi hizo.

"Kwa dhati kabisa naupongeza uongozi wa Shule ya Feza kwa kuwa taasisi ya mfano na ya kipekee katika kutoa elimu bora kwa miaka mingi hapa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla," alisema.

Alisema faraja yake ni kuona ufaulu mzuri wa wanafunzi ambao unasababisha kupata fursa mbalimbali za kujiunga na vyuo vikuu vya ndani na nje ya nchi.

Hemed aliwaasa wahitimu hao kuwasikiliza na kuwatii wazazi wao pamoja na kuthamini juhudi za walimu waliojitahidi katika makuzi yao.

Naye Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Muhamed Mussa, alisema kuwa Shule ya Feza ni miongoni mwa shule zinazofanya vizuri nchini jambo ambalo linasaidia kupata wasomi wazuri wanaotegemewa na taifa.

Aidha, alisema sekta ya elimu inakabiliwa na changamoto nyingi na shule hiyo imekuwa mstari wa mbele kukabiliana nazo kwa lengo la kupata wataalamu bora wenye nidhamu, maadili na uzalendo.

Akisoma risala ya wahitimu mwanafunzi, Mudrik Salum, aliushukuru uongozi wa shule hiyo kwa kuwajenga kifikra za kitaaluma na wamewahakikishia kuendeleza mema yote waliyofunzwa wakiwa shuleni hapo. Akitoa shukrani kwa niaba ya wazazi wa wanafunzi waliohitimu, Amria Masoud Ali, aliwashukuru walimu wa shule hiyo kwa kuwasimamia watoto wao katika taaluma na malezi na kueleza imani yake kuwa wahitimu hao watakuwa kioo kwa jamii pamoja na kuwa taifa bora.

## ACT-Wazalendo yatoa msimamo Muungano

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha ACT- Wazalendo Zanzibar, Othman Masoud Masoud, amesema kwamba msimamo wa chama hicho ni kuwapo Muungano wenye fursa sawa kwa pande mbili za Muungano ambao utakuwa na manufaa ya kimaendeleo kwa kila upande.

Othman aliyasema hayo alipozungumza na ngome ya vijana ya chama cha ACT, Kiembesamaki kwa nia ya kuwakumbusha vijana kuhusu madhumuni ya kuendelea na harakati za kudai mabadiliko ya Muungano.

Alisema Muungamo wa sasa wa serikali mbili hauwezi kuwa salama na wenye manufaa kwa Zanzibar na kwa hivi sasa ulivyo unaonekana kuunufaisha zaidi upande wa Tanzania na suluhisho pekee ni kuwapo Muungano wa serikali tatu ambao utatenganisha mambo ya Zanzibar na Tanganyika.

Alisema kwa mfumo uliopo sasa ambao hauna utaratibu wa uwajibikaji na kiongozi anaweza akafanya atakavyo bila kuwapo chombo cha kumuwajibisha na hivyo nchi haiwezi kusonga mbele.

Othman ambaye pia ni Makamu wa Kwanza wa Rais, alisema mfumo wa sasa wa serikali mbili sambamba na katiba iliyopo haitoi nafasi na haki kwa Zanzibar kuwa na mamlaka ya kuchagua Rais wa Muungano ambaye anapatikana kwa wingi wa kura jambo ambalo halitoi uzito wa haki kwa Zanzibar.

Alisema mfumo wa Muungano uliopo sasa una upungufu mkubwa hata katika utaratibu wa kisheria, kutokuwapo sera ya kusimamia mambo ya Muungano na pia kwenye nyenzo za kiuchumi kusimamiwa na upande mmoja huku Zanzibar ikibakia imefungwa mikono.

Kadhalika, alisema dhamira ya chama hicho ni kupigania pia kuondoa utaratibu wa nchi kuongozwa kwa mfumo wenye matakwa na maslahi ya kundi ama watu fulani na badala yake kuwapo serikali inayowajibika kwa wananchi kwa maslahi ya taifa.

Alisema hali hiyo itawezekana iwapo nchi itaandaa na kuwa na uchaguzi huru na wa haki wa kuweza kuwapata viongozi mbali mbali ambao watejenga nidhamu bora ya kuwajibika kwa wananchi.

Akizungumzia Serikali ya Umoja wa Kitaifa, Othman alisema kwamba chama chake kimeingia katika serikali hiyo kwa nia ya kupigania mabadiliko kwa kuweka misingi bora ya utekelezaji wa serikali hiyo kuwa imara kwa maslahi ya taifa. Alisema kuwa uamuzi wa chama chake ni kupigania mabadiliko ya kuwapo serikali ya kweli ya Umoja wa Kitaifa kwa kuwa iliyopo kwenye Katiba hivi sasa ni fursa pekee ya kujenga misingi ya serikali hiyo ili kuijenga vyema Zanzibar.

Naye Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama hicho Ismail Jussa Ladhu, aliwataka vijana kutovunjika moyo na badala yake kuendelea na vugugugu la harakati za kujenga chama na kuitafutia Zanzibar mamlaka kamili.

Alisema kwamba viongozi wailiaosisi chama hicho hawakuwa na uroho wa madaraka na ndiyo maana waliweza kusamehe mararaka na vyeo vikubwa walivykuwa navyo lakini kwa sababu ya uzalendo wa kupigania nchi hawakujali madaraka.

Mwenyekiti wa Ngome ya Vijana ya ACT –Taifa, Abdul Nondo, alisema katika kuimarisha muungano wenye kutoa haki kwa pande zote ni lazima kushughulikiwa kwa umakini changamoto za muungano ikiwa ni pamoja na kuwepo katiba mpya inayozingatia kuondosha kero za Muungano.

# KIOO Limited yatwaa tuzo mwajiri bora 2022

**Na Joseph Mwendapole**

KAMPUNI ya KIOO Limited imetwaa tuzo ya mwajiri bora inayotolewa na Chama cha Wafanyakazi wa Sekta ya Biashara, Taasisi za Fedha, Huduma na Ushauri (TUICO), Kanda ya Das es Salaam.

Tuzo hizo zilikabidhiwa mwishoni mwa wiki na Katibu Mkuu TUICO, Boniface Nkakatisi na kupokelewa na Meneja Rasilimali Watu, Jacob Msuya.

Msuya, aliipongeza TUICO kwa tuzo hiyo itakayoongeza chachu ya utendaji kazi kwenye kampuni.

Alisema ushindi huo unatokana na wanavyowajali wafanyakazi wao na kuthamini maslahi yao.

Alisema kuzingatia maslahi ya wafanyakazi na kuwawekea mazingira mazuri ya kazi watumishi wake, imekuwa chanzo kikubwa cha kampuni hiyo kushika nafasi hiyo ya kwanza kwa mwaka wa pili mfululizo.

Pia, kampuni hiyo ina tatua changamoto za ndani za wafanyakazi na menejimenti, jambo lililochangia kujenga uhusiano mzuri na wafanyakazi wake.

"Tunathamini sana wafanyakazi na tumewawekea mazingira rafiki na salama ya kufanyakazi wafanyakazi wetu na tunafanya haya kuunga mkono juhudi za serikali yetu kuhakikisha Tanzania inakuwa nchi ya viwanda," alisema.

Akizungumza kwenye hafla hiyo, Katibu wa TUICO Temeke, Magwe Muyaga, alisema miongoni mwa mafanikio makubwa ya chama hicho ni kutatua migogoro mbalimbali ya wafanyakazi.

Alisema TUICO imefanikiwa kutatua migogoro 247 na kufanikiwa kuendeleza uhusiano mwema baina ya waajiri na wafanyakazi na kutoa elimu kuhusu masuala mbalimbali kwa wanachama wake.

Kuhusu changamoto, alisema kuna baadhi ya waajiri wakorofi wanaowakataza wafanyakazi kujiunga na chama hicho, pia kuwakataza washiriki mikutano ya chama hicho kwa kisingizio cha ugonjwa wa UVIKO-19, hivyo kukwamisha shughuli zao.



Mkuu wa Wilaya ya Iringa Mohamed Moyo (wa pili kushoto) akiwa na wajumbe wa kamati ya siasa ya Wilaya ya Iringa vijijini walipofanya utalii katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

# Wafanyabiashara wa mkaa wang'ang'aniwa tozo 250/-

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, amewataka wafanyabiashara wa mkaa kuendelea kulipa tozo za mazao ya misitu zilizowekwa kwa mujibu wa sheria.

Kunenge alitoa agizo hilo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu malalamiko ya wafanyabiashara hao kulipa ushuru wa bidhaa hiyo kuwa ni kubwa.

Alisema tozo ya Sh. 250 kwa kilo ya mkaa inatozwa kwa mujibu wa sheria GN 59 ya Januri 28, 2022 iliyotolewa na waziri mwenye dhamana.

Kunenge alisema kumekuwa na vikwazo namna ya kukusanya tozo hiyo jambo ambalo mkoa huo umeanza kulishughulikia kwa kuandaa mapendekezo yake kwa ajili ya kuyafikisha kwenye wizara husika.

"Tumewaita kutoa ufafanuzi na maelekezo kuhusu tozo za mazao ya misitu kwa bidhaa ya mkaa, kimsingi viwango vya tozo ni Sh. 250 kwa kila kilo ya mkaa vimewekwa kufuatia GN 59 iliyotolewa na Waziri mwenye dhamana hivyo haviwezi kubadilika bila kufuata taratibu," alisema.

"Sheria ya maelekezo ya tozo hiyo ipo kwenye Gazeti la Serikali na ilitolewa na waziri mwenye dhamana utaratibu huo utaendelea haya masuala ya kisheria yana namna yake ya kuyafanyia mabadiliko," alisema.

Alisema Serikali ya Mkoa huo imeandaa mapendekezo kuhusu tozo ya mkaa na watayawasilisha kwa waziri husika ili aweze kuyapitia na kuyafanyia kazi.

"Wafanyabiashara waendelee kulipa kiasi hicho hadi pale serikali itakapotoa taarifa itakavyoona inafaa kuwa na mabadiliko kwani mkoa umeona kikwazo kilichopo kwenye tozo hizo na umeshaandaa mapendekezo hatua zinaendelea kumfikia waziri," alisema.

Aliwataka wakazi wa mkoa huo kujikita kwenye matumizi ya nishati mbadala na kuacha kutegemea mkaa.

# RUNAPA yaweka mkakati kutangaza utalii

**Na Friday Simbaya,** IRINGA

HIFADHI ya Taifa ya Ruaha (RUNAPA) mkoani Iringa katika mkakati wake wa kutangaza utalii Kanda ya Kusini, inatarajia kuanzisha mkataba maalum wa utalii katika eneo la Kusini mwa Hifadhi ya Usangu.

Hayo yamesemwa hivi karibuni na Ofisa Utalii wa RUNAPA, Amina Salum, alipokuwa akitoa taarifa kwa kamati za siasa za CCM wilaya (Manispaa ya Iringa na Iringa DC), zilipotembelea hifadhi hiyo na kuongozwa na Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Mohamed Moyo.

Kamati za siasa za wilaya (Manispaa na Iringa Vijijini) zilitembelea hifadhi hiyo na kutangaza utalii ili kuleta matokeo chanya katika maendeleo ya utalii katika hifadhi hiyo.

Salum alifafanua kuwa eneo la mikataba ya utalii (tourism concession area) ni aina ya uwekezaji utakaomwezesha mwekezaji kuruhusiwa kuwa na eneo maalum ndani ya hifadhi ya taifa, chini ya uangalizi wa mwekezaji kwa kutoa huduma kwa wageni.

Pia, mkakati huo utamtaka mwekezaji kuwa na mtaji mkubwa wa ujenzi wa majengo, vifaa na gharama za uendeshaji na utamruhusu kutoa huduma za malazi, chakula na vinywaji, elimu na shughuli za utalii.

Aidha, mkataba maalum wa utalii wa kipekee utamtaka mwekezaji kulipa tozo maalum ya mwaka mzima.

RUNAPA imetenga maeneo mbalimbali ya uwekezaji kwa ajili ya kujenga nyumba za kulala wageni, kambi za kudumu za mahema, kambi maalum za msimu, safari za puto, hosteli na nyumba ndogo pamoja na kujenga kambi za umma.

Alisema katika mikakati mingine ya kukuza utalii wanakusudia kuanzisha aina mpya za utalii ambazo ni safari za boti, wapanda farasi, kutenga maeneo zaidi ya kambi za wageni, kutoa huduma kwa mujibu wa mfumo wa kimataifa wa usimamizi wa ubora (QMS) kutoka Shirika la viwango vya kimataifa (ISO 9001).

Vile vile, kusimamia na kutekeleza miongozo ya shirika ya kukabiliana na ugonjwa wa COVID-19 pamoja na kufungua miundombinu ya utalii kupitia mradi wa maeneo yaliyohifadhiwa (REGROW) ili kuwawezesha wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza kwenye hifadhi.

Hifadhi ya Taifa ya Ruaha ina jumla ya wawekezaji 13 ambao wamewekeza katika kambi za mahema, nyumba za kulala wageni na kambi za muda zenye vitanda 296.

## Watu 30 wafariki katika mkanyagano Nigeria

**ABUJA,** NIGERIA

ZAIDI ya watu 30 wameuwawa kusini mwa Nigeria juzi Jumamosi katika mkanyagano uliozuka wakati wa hafla ya kugawa chakula kanisani.

Viatu vilitapakaa baada ya tukio hilo katika eneo la Port Harcout kusini mwa Nigeria, ambapo kanisa moja lilitoa chakula na zawadi kwa wasiojiweza lakini umati uliingilia kati na kusambaratisha zoezi hilo.

Kulingana na taarifa ya polisi Jumla ya watu 31 walipoteza maisha katika mkanyagano huo na kwamba uchunguzi unaendelea.

Nigeria imeshuhudia majanga kadhaa ya mkanyagano katika maeneo ya usambazaji wa chakula katika miaka ya hivi karibuni, ikiwa ni pamoja na mpango wa chakula wa shirika la misaada kaskazini mwa Jimbo la Borno, na kusababisha wanawake saba kufa mwaka jana.



## Uhasama Rwanda, Congo wazidi kufukuta

**KIGALI,** RWANDA

RWANDA imesema wanajeshi wake wawili wanazuiliwa na waasi katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, na kuishutumu serikali ya Congo kwa kuunga mkono kundi lililohusika.

Haya yanajiri wakati mgogoro wa kidiplomasia ukiendelea kufukuta kati ya majirani hao huku pande zote mbili zikilaumiana kusaidia wanamgambo wenye silaha katika eneo lenye hali tete mashariki linalopakana na Rwanda.

Juzi shirika la ndege la RwandAir lilitangaza kusitisha safari zake kuelekea Jamhuri ya Kidemkrasia ya Congo.

Hata hivyo, Congo ilisimamisha ndege hiyo na kumshutumu balozi wa Rwanda kwa kile inachodai kuwa Rwanda inawaunga mkono waasi wa kundi la M23.

# Russia yaongeza mashambulizi Ukraine

**KYIV,** UKRAINE

VIKOSI vya Russia vimeongeza kasi ya mashambulizi dhidi ya mji wa Sievierodonetsk mashariki mwa Ukraine baada ya kuutia mkononi mji wa Lyman.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka eneo hilo, wanajeshi wanakaribia kuliteka eneo lote la Luhansk katika jimbo la Donbas, kwenye vita, ambavyo sasa vimeingia katika mwezi wake wa nne tangu kuanza Februari.

Wizara ya ulinzi ya Russia ilisema wanajeshi wake pamoja na vikosi vya washirika vya waasi wanaotaka kujitenga sasa vinaudhibiti kikamilifu mji wa Lyman.

Eneo hilo ni muhimu kutokana na kuwa na makutano ya huduma za reli kutoka magharibi mwa mto Siverskyi Donets katika mkoa wa Donetsk ambao ni jirani na mkoa wa Luhansk.

Hata hivyo naibu waziri wa ulinzi wa Ukraine, Hanna Malyar alisema vita katika mji huo wa Lyman bado viliendelea.

Polisi walichapisha kwenye mitandao ya kijamii siku ya Jumamosi kwamba mji wa Sievierodonetsk umekabiliwa na mashambulio makali ya vikosi vya Russia.

**Maofisa wa Marekani wameliambia shirika la Habari la Reuters kwamba ombi la Ukraine linazingatiwa na uamuzi utatolewa katika siku zijazo.**

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa eneo la Lysychansk-Bakhmut, pia limekabiliwa na mashambulizi makali ambapo majeshi ya Russia yanalenga kuuchukua ili kuweza kuvizingira vikosi vya Ukraine.

Polisi ya Ukraine imesema kumetokea uharibifu mkubwa katika mji huo wa Lysychansk.

Mshauri wa rais wa Ukraine ambaye pia anaiwakilisha nchi yake kwenye mazungumzo ya amani, Mykhailo Podolyak, alitoa wito huo kwa nchi yake kupewa magari ya kijeshi yanayoweza kurusha makombora mengi ya masafa marefu kwa wakati mmoja kutoka Marekani.

Maofisa wa Marekani wameliambia shirika la Habari la Reuters kwamba ombi la Ukraine linazingatiwa na uamuzi utatolewa katika siku zijazo.

Rais wa Ukraine Volodymyr Zelenskiy, ameonyesha matumaini katika hotuba yake kwa njia ya video kwamba washirika wataipa nchi yake silaha zinazohitajika kufikia wiki ijayo.

Zelenskiy alisema haamini wazo la kutumia nguvu ili kuikomboa ardhi yote iliyonyakuliwa na Russia tangu mwaka 2014, ambayo pia inajumuisha jimbo la Crimea.

Katika juhudi za kidiplomasia kuwezesha kupatikana suluhu kwenye vita vya Ukraine Rais wa Ufaransa Emmanuel Macron na Kansela wa Ujerumani Olaf Scholz walizungumza kwa njia ya simu na Rais wa Russia Vladimir Putin siku ya Jumamosi ambapo walimuhimiza juu ya kuondoa vizuizi kwenye bandari ya Odesa na kuruhusu usafirishaji wa nafaka kutoka Ukraine.

Viongozi hao walisema rais Putin aliwaambia kwamba nchi yake iko tayari kujadili njia zitakazoiwezesha Ukraine kuanza tena usafirishaji wa nafaka kutoka kwenye bandari zake katika Bahari Nyeusi.



Moshi ukiwa umetanda katika anga la mji wa Sievierodonetsk kutokana na mashambulizi makali ya makombora yanayofanywa na vikosi vya Russia. **PICHA: DW**

## Viongozi Umoja wa Afrika wajadili ugaidi

**MALABO,** EQUATORIAL GUINEA

VIONGOZI wa Umoja wa Afrika wamejadili kuhusu ugaidi na vitisho vya itikadi kali katika siku ya pili ya mkutano wa kilele wa umoja huo nchini Equatorial Guinea.

Mkutano huo uliitishwa kufuatia msururu wa mapinduzi katika bara hilo, na mabadiliko ya kikatiba ya serikali.

Nchi nyingi za Kiafrika pia zinakabiliwa na mashambulizi ya kigaidi pamoja na changamoto zinazohusiana na chakula na maji kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa.

Mkuu wa kamati kuu la Umoja wa Afrika Moussa Faki Mahamat, alisema karibu Waafrika milioni 113 wanahitaji msaada wa haraka wa kibinadamu mwaka huu.

Idadi hiyo pia inajumuisha wakimbizi milioni 48, wanaotafuta hifadhi, pamoja na wakimbizi wa ndani. Wanachama wanne wa Umoja wa Afrika, ikiwamo Guinea, Burkina Faso, Sudan na Mali kwa sasa wamesimamishwa kutoka mapinduzi ya kijeshi au kutokuwepo kwa serikali ya kiraia

Matukio ya mashambulizi ya silaha yameongoza kusababisha vifo nchini humo kuliko ajali za gari kwa mwaka 2020. **BBC**

HABARI MICHEZO

# Z'BAR QUEENS YATUA UGANDA TAYARI KUIVAA ETHIOPIA CECAFA

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Soka ya Taifa ya Wanawake Zanzibar 'Zanzibar Queens', imeondoka jana Jumapili, kuelekea nchini Uganda katika michuano ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), kwa Wanawake.

**Timu hiyo imeondoka mjini Zanzibar jana kwa boti kupitia Dar es Salaam na kisha kusafiri kwa basi kuelekea Uganda ikiwa na msafara wa watu 29 kati yao wachezaji wakiwa 20 na viongozi tisa, ambapo inatarajiwa kuwasili nchini humo leo, Jumatatu.**

Zanzibar katika michuano hiyo ya CECAFA imepangwa Kundi B pamoja na Tanzania Bara, Sudan Kusini na Ethiopia, wakati Kundi A likiundwa na wenyeji Uganda, Burundi, Rwanda na Djibouti.

Michuano hiyo inatarajiwa kuanza Jumatano wiki hii kwa Burundi kuvaana na Djibouti kabla ya Uganda kupepetana na Rwanda, wakati Zanzibar Queens itaanza kutupa karata yake ya kwanza Alhamisi wiki hii dhidi ya Ethiopia na siku hiyo hiyo Tanzania Bara ikimenyana na Sudan Kusini.

Awali, juzi usiku akikabidhi bendera kwa timu hiyo ya Taifa ya Wanawake, Katibu Mkuu wa Baraza la Michezo la Taifa Zanzibar (BTMZ), Marine Said, aliwataka wachezaji hao kutunza nizamu ili waweze kufanikiwa.

Alisema mafanikio yoyote katika sekta ya michezo yanapatikana kwa kutunza nizamu, umoja pamoja na ushirikiano kwa wote.

Aidha, alisema anaimani kubwa na timu hiyo kufanya vizuri japokuwa haikuwa na maandalizi makubwa sana, lakini wachezaji walipata mazoezi ya pamoja kwa muda mrefu.

"Tunawategemea mtabadilika, tunawategemea mabadiliko zaidi yatakuwapo katika kutunza nidhamu kwa muda wote, muheshimu hata mpinzani wako uwanjani, muheshimu kiongozi yeyote ambao mtakutana nao katika michuano hii hata kama hatukufanikiwa katika kushindanda uwanjani, lakini tutashinda katika nizamu naomba zingatieni hili," alisema.

Kwa upande wa nahodha wa timu hiyo, Mwajuma Abdallah, aliwaahidi Wazanzibar kuwa timu hiyo itafanya vizuri ikilinganishwa na mashindano yaliyopita.



Katibu Mkuu wa Baraza la Michezo la Taifa Zanzibar (BTMZ), Marine Said (wa pili kulia), pamoja na viongozi mbalimbali wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), wakikabidhi Bendera ya Taifa kwa Nahodha wa Zanzibar Queens, Mwajuma Abdallah (katikati), juzi visiwani Zanzibar, tayari kwa ajili ya kwenda kuipeperusha vema kwenye michuano ya CECAFA nchini Uganda. **PICHA: HAWA ABDALLAH**

# *Netiboli Ligi Daraja la Kwanza kupigwa Dar*

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Chama cha Netiboli Tanzania (CHANETA), umehamisha kituo cha Ligi Daraja la Kwanza na sasa ligi hiyo itafanyika Dar es Salaam, imeelezwa.

Awali, ligi hiyo ilipangwa kufanyika jijini Mbeya na sasa itafanyika Dar es Salaam kwenye uwanja wa ndani wa Benjamin Mkapa (Indoor Taifa) kuanzia Julai 9-17, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jaana, Katibu Mkuu wa CHANETA, Rose Mkisi, alisema hatua ya kubadilisha kituo ni kutokana na ushauri wa Baraza la Michezo Taifa (BMT), kuhakikisha ligi hiyo inafanyika Dar es Salaam kwa ajili ya kupata wadhamini watakaosaidia kila kitu kwenda vizuri.

Alisema maandalizi yanaendelea vizuri kiufundi na miundombinu tayari ipo sawa na kwamba barua zimezifikia timu shiriki kwa ajili ya mabadiliko ya kituo cha ligi hiyo.

"Nipende kuwaambia, tumehamisha kituo sasa tutafanyia Dar es Salaam kutokana na kwamba tunajitangaza na ligi hii kubwa tumeona tuombe Azam waturushi mubashara ili mchezo wetu utambulike urudi katika mstari," alisema Rose.

Alisema wanatarajia kuwa na timu 29 za wanawake na wanaume zitakazoshiriki ligi hiyo, na kwamba 27 zimethibitisha kushiriki na kati ya hizo 21 ni wanawake 21 na wanaume sita.

Alizitaja timu za wanawake kuwa ni Tamisemi, Uhamiaji, JKT Mbweni, Mgulani JKT, Jeshi Stars, Magereza Morogoro, Eagle Queens, Kampala na Makutupora Dodoma.

Nyingine ni Polisi Arusha, Polisi Kigoma, Polisi Tanga, Polisi Morogoro, MRVF Dream, Mbozi United, Mbeya City, Chuo Kikuu Dar es Salaam (UDSM), Tarime Queens, Jiji Tanga, Jiji Arusha na Mabibo Queens.

Kwa wanaume ni Smart Boys, Hapa Kazi, Muungano Dodoma, Jiji Arusha, Bright Dodoma na Ushirika Moshi.

# Ethiopia U-18 na 20 zashinda riadha Dar

**Na Saada Akida**

TIMU za Taifa za Ethiopia za michezo ya Riadha chini ya umri wa miaka 18 na 20 (U-18 na 20), zimefanikiwa kutwaa ubingwa katika mashindano ya Afrika Mashariki yaliyomalizika juzi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Mashindano hayo ya siku mbili yalianza Mei 27-28, mwaka huu, huku yakishirikisha nchi saba ambazo ni, Zanzibar, Ethiopia, Kenya, Eritrea, Sudan Kusini, Somalia na wenyeji Tanzania Bara.

Tanzania Bara wamemaliza nafasi ya tano huku U-20, wakichukua medali moja ya dhahabu, tatu za fedha na nne za shaba na timu ya U-18 ikiambulia medali ya fedha moja na tano za shaba.

Kwa upande wa visiwani Zanzibar, timu U-20 imemaliza nafasi ya tatu kwa kuondoka na medali mbili za dhahabu, fedha mbili na shaba moja na chini ya miaka 18 wameshika nafasi ya pili kwa kushinda medali tatu za dhahabu, tatu fedha na mbili shaba.

Timu ya vijana ya U-20 ya Kenya, imemaliza nafasi ya pili kwa kuondoka na medali nne za dhahabu na tano za fedha huku kwa upande wa U-18 wakiwa nafasi ya tatu kwa kushinda medali moja ya dhahabu, nne fedha na moja shaba.

Eritrea imemaliza mashindano hayo wakiwa nafasi ya nne kwa ujumla kwa upande wa timu ya U-20 na U-18, kwa kuondoka na medali mbili za dhahabu, fedha moja na shaba mbili.

Kwa upande wa U-18 hawakuwa na dhahabu bali walishinda medali mbili za fedha na moja shaba,

Mshindi wa sita umeenda kwa timu ya Sudan Kusini kwa timu zote mbili U-18 na U-20 kuondoka na medali mbili, moja ikiwa ya fedha na nyingine shaba wakati wa U-20 wakiambulia fedha mbili.

Somalia imeburuza mkia kwa kutopata medali yoyote katika mashindano hayo yaliyomaliza juzi.

Rais wa Shirikisho la Riadha Tanzania, Silas Isangi, amewapongeza wanariadha kwa kiwango walichoonyesha ingawa maandalizi hayakuwa ya muda mrefu kwa timu ya Tanzania.

"Wito wangu kwa wanariadha kujituma kufanya mazoezi na kufuata maelekezo ya walimu wao ili waweze kutimiza ndoto zao kwa kuwa michezo kwa sasa ni ajira na afya," alisema Silas.

## ZISIKUPITE

### KANTE AWINDWA UNITED

KLABU ya Manchester United inafikiria kuwasilisha ombi la kumnunua kiungo wa kati wa Chelsea na Ufaransa, N'Golo Kante, 31. ***(Guardian)***

### DEMBELE ATAKIWA LIVER

LIVERPOOL wamefanya mawasiliano na winga wa Ufaransa, Ousmane Dembele, 25, ambaye mkataba wake na Barcelona unamalizika msimu huu wa majira ya joto. ***(Sport)***

### TUCHEL AMTAKA GALLAGHER

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel atafanya mazungumzo na kiungo wa kati wa England, Conor Gallagher, 22, kabla ya kuamua mustakabali wake. Msimu uliopita alicheza kwa mkopo Crystal Palace. ***(Fabrizio Romano)***

### GUNDOGAN ASUBIRIWA CITY

NYOTA wa Manchester City, Ilkay Gundogan, 31, anasubiriwa kuzungumzia nafasi yake.***(90min)***

### KOMPANY NA BELLIS

KOCHA mtarajiwa wa Burnley, Vincent Kompany anataka kumfanya beki wa kati, Taylor Harwood-Bellis, 20, kuwa usajili wake wa kwanza pale dimba la Turf Moor kwa mkopo kutoka klabu ya zamani ya Manchester City. ***(TSun)***

### RAPHINHA AMULIKWA BARCA

BABA wa winga wa Leeds United, Raphinha, 25, amesema "uwezekano upo" juu ya mustakabali wake huku mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil akiendelea kuhusishwa na Barcelona. ***(Express)***

### DI MARIA MWAKA MMOJA

KLABU ya Juventus imempa mkataba wa mwaka mmoja winga wa Argentina, Angel di Maria, 34, baada ya kuamua kuondoka PSG mwishoni mwa msimu huu. ***(Calciomercato)***

### CAVANI AIOTA UNITED

MSHAMBULIAJI wa Uruguay, Edinson Cavani, 35, amesema amebakiwa na "ladha chungu" katika barua ya wazi kwa Manchester United baada ya kuondoka katika klabu hiyo. ***(Star)***

### PERISIC HUYOOO SPURS

WINGA wa Croatia, Ivan Perisic, 33, anatarajiwa kusaini mkataba wa kujiunga na Tottenham Hotspur kutoka Inter Milan kwa uhamisho huru na mpango huo unaweza kutangazwa wiki ijayo. ***(Fabrizio Romano)***

### DYBALA KWA MOURINHO

KOCHA wa AS Roma, Jose Mourinho anatumaini kuzishinda klabu zake za zamani, Tottenham Hotpur na Manchester United katika kumsajili mshambuliaji wa Argentina, Paulo Dybala, 28, kwa uhamisho huru baada ya kuondoka Juventus msimu huu wa majira ya joto. ***(TyC Sports, via Express)***

### RICHARLISON AWINDWA PSG

KLABU ya Paris St-Germain inataka kumsajili mshambuliaji wa Brazil, Richarlison, 25, kutoka Everton msimu huu wa majira ya joto. ***(Fichajes)***

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# KLOPP: MSIHOFU TUTAKUWA KWENYE FAINALI IJAYO UEFA

●●● Nina hisia kubwa kwamba tutarudi tena, msimu ujao Istanbul? Weka nafasi ya hoteli...

**PARIS,** Ufaransa

KOCHA Jurgen Klopp, amewaambia mashabiki wa Liverpool kujiandaa "kuomba nafasi ya hoteli" kwa ajili ya fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka ujao kule Istanbul.

**Real Madrid iliifunga Liverpool 1-0 katika fainali iliyofanyika jijini Paris juzi Jumamosi na kuwanyima 'Wekundu' hao kutwaa taji la pili la michuano hiyo ndani ya miaka mitatu.**

Ina maana wanamaliza msimu huu wakiwa wameshinda Kombe la FA na Kombe la Corobao.

"Nina hisia kubwa kwamba tutarudi tena. Vijana wana ushindani. Tutakuwa na kundi bora msimu ujao," alisema Klopp akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

"Iko wapi (mwisho) msimu ujao? Istanbul? Weka nafasi ya hoteli."

Wiki moja kabla ya kipigo cha Jumamosi, bado kulikuwa na gumzo la Liverpool kuweza kushinda mataji manne kwa vile walikuwa kwenye mbio za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu England.

Hilo lilipunguzwa hadi kufikia mataji matatu Jumapili ya wiki moja iliyopita wakati Manchester City ilipotwaa ubingwa siku ya mwisho ya msimu wa Ligi Kuu England.

Liverpool walipata nafasi nyingi katika kipindi cha kwanza dhidi ya Real kwenye Uwanja wa Stade de France, lakini mlinda mlango Thibaut Courtois alikuwa kwenye kiwango cha hali ya juu.

Wakati Wekundu hao wakikamilisha msimu kwa mataji mawili, Klopp alikiri ilikuwa mapema sana kwa wachezaji wake kuweza kuthamini kuwa wamefanikiwa.

"Kwenye chumba cha kubadilishia nguo hakuna anayehisi ulikuwa msimu mzuri kwa sasa," alisema Klopp.

"Labda tunahitaji masaa machache kwa hilo. Tulicheza mchezo mzuri, sio mchezo kamili. Vijana walijaribu kila kitu, haswa tukiwa nyuma kwa bao 1-0, kisha tukacheza kama tulivyotaka kucheza hapo awali."

LIVE IN PLAY

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 233,

MECHI KALI

AL AHLY CAIRO

VERSUS

WYDAD CASABLANCA

1 | 3.01

X | 2.86

2 | 2.39

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa

SPORTPESA.CO.TZ

HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MARCELO RASMI KUONDOKA MADRID




**PARIS,** Ufaransa

MLINZI mkongwe wa Brazil, Marcelo, amethibitisha kuwa anaondoka Real Madrid baada ya kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Beki huyo wa kushoto mwenye umri wa miaka 34, amekuwa na 'Los Blancos' hao tangu mwaka 2007, akicheza mechi 550 akiwa na klabu hiyo.

Marcelo, ambaye hakutumika kama mchezaji wa akiba katika ushindi wa 1-0 Jumamosi dhidi ya Liverpool, alithibitisha baada ya mchezo huo kwamba ataondoka kwenye klabu hiyo msimu huu baada ya mkataba wake kumalizika mwishoni mwa Juni.

Alisema: "Ilikuwa mechi yangu ya mwisho na Real Madrid".

Marcelo ataondoka katika klabu hiyo akiwa na mataji 25, ambayo ni zaidi ya mchezaji mwingine yeyote katika historia ya klabu hiyo.

Kulikuwa na uvumi kwamba Mbrazil huyo anaweza kukubali kukatwa mshahara ili kubakia Madrid msimu ujao.

Marcelo, ambaye alijiunga na Madrid kutoka Fluminense, alicheza mechi 18 katika mashindano yote msimu huu.




## Aubameyang aisikitikia Arsenal

**BARCELONA,** Hispania

PIERRE -Emerick Aubameyang amesema alisikitishwa na kushindwa kwa Arsenal kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya, kwani alitarajia kukutana na klabu yake hiyo ya zamani akiwa na Barcelona.

Licha ya kufurahia msimu wa kutia moyo chini ya kocha Mikel Arteta, Arsenal ilikosa nafasi ya nne bora mbele ya wapinzani wao wa jiji moja, Tottenham Hotspur baada ya kupoteza mechi zao mbili kati ya tatu za mwisho wa msimu wa Ligi Kuu England.

Kuporomoka kwao mwishoni mwa msimu kulimaanisha Arsenal haijamaliza katika nafasi nne za juu za Ligi Kuu tangu 'Washikabunduki' hao walipomaliza wa pili mbele ya Leicester City msimu wa 2015-16 wakiwa chini ya kocha Arsene Wenger.

Aubameyang, kwa upande wake, aliondoka pale Uwanja wa Emirates Januari baada ya miaka minne katika klabu hiyo, akifunga mabao 13 katika mashindano yote akiwa na Xavi ya Barcelona huku 'Blaugrana' hao wakimaliza nafasi ya pili kwenye LaLiga.

Mshambuliaji huyo raia wa Gabon, amekuwa mfungaji bora wa pamoja wa Barca kwenye msimu huu pamoja na Memphis Depay, licha ya kucheza mechi 23 pekee tangu alipowasili Camp Nou.

,880,320

# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 01/06/22 | 21:45 | Scotland vs Ukraine | 2.27 | 3.13 | 3.33 |
| 02. 01/06/22 | 21:45 | Italy vs Argentina | 2.82 | 3.02 | 2.41 |
| 03. 01.06.22 | 23:00 | Real Cartagena vs Leones FC | 2.68 | 3.02 | 2.53 |
| 04. 02.06.22 | 02:30 | Fortaleza CE vs Ceara CE | 2.24 | 3.16 | 2.97 |
| 05. 02.06.22 | 02:30 | USA vs Morocco | 2.24 | 3.18 | 3.33 |
| 06. 02.06.22 | 03:30 | CRB AL vs CSA AL | 2.39 | 2.91 | 2.96 |
| 07. 02.06.22 | 19:00 | Bulgaria vs North Macedonia | 2.54 | 2.98 | 2.93 |
| 08. 02.06.22 | 19:00 | Cyprus vs Kosovo | 3.25 | 3.15 | 2.25 |
| 09. 02.06.22 | 21:45 | Czech Republic vs Switzerland | 2.90 | 3.25 | 2.39 |
| 10. 02.06.22 | 21:45 | Spain vs Portugal | 2.24 | 3.25 | 3.15 |
| 11. 02.06.22 | 21:45 | Serbia vs Norway | 2.27 | 3.10 | 3.25 |
| 12. 02.06.22 | 21:45 | Slovenia vs Sweden | 3.21 | 3.11 | 2.29 |
| 13. 02.06.22 | 21:45 | Northern Ireland vs Greece | 2.85 | 3.00 | 2.60 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMATATU - 30/05/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 2900 | FC Tuapse vs Spartak Nalchik | 3.40 | 2.92 | 2.16 |
| 13:00 | 5965 | Mohammedan Sporting Club Dhaka vs Bashundhara Kings | 5.64 | 3.79 | 1.52 |
| 16:00 | 3747 | Selangor Pkns vs Kuching FA | 2.65 | 3.20 | 2.60 |
| 16:00 | 4017 | Polisi Tanzania vs Biashara United | 2.34 | 2.56 | 3.53 |
| 17:00 | 1443 | Villa San Carlos vs Satsaid | 3.07 | 3.80 | 1.96 |
| 17:00 | 3838 | Vard Haugesund vs Odds BK 2 | 1.55 | 4.09 | 4.77 |
| 18:00 | 1900 | FCI Levadia Tallinn U21 vs Paide Linnameeskond | 2.79 | 4.19 | 2.11 |
| 18:30 | 2482 | Pepo Lappeenranta vs KPV Kokkola | 2.54 | 3.37 | 2.44 |
| 18:30 | 2586 | FC KTP vs EIF Ekenas | 1.82 | 3.55 | 3.74 |
| 18:30 | 3378 | Kapa vs Kiffen | 2.34 | 3.63 | 2.52 |
| 19:00 | 1051 | SuperSport Utd vs Orlando Pirates | 3.91 | 3.42 | 1.88 |
| 19:00 | 1250 | Brann vs Mjondalen | 1.36 | 4.65 | 6.78 |
| 19:00 | 2424 | Grorud IL vs Stjordals-Blink | 1.95 | 3.61 | 3.22 |
| 19:00 | 2995 | Komeetat vs FC Vaajakoski | 3.80 | 4.50 | 1.71 |
| 19:00 | 3119 | Kfum Oslo vs Skeid Fotball | 1.52 | 4.09 | 5.06 |
| 19:00 | 3489 | Flora II vs Parnu Jalgpalliklubi | 1.51 | 4.39 | 5.59 |
| 19:00 | 4283 | Raufoss vs Aasane Fotball | 1.86 | 3.69 | 3.45 |
| 19:00 | 4665 | Stabaek vs Kongsvinger IL | 1.39 | 4.49 | 6.44 |
| 19:30 | 5840 | Spjelkavik vs Molde FK 2 | 2.41 | 4.38 | 2.19 |
| 19:30 | 5850 | National Bank vs Ceramica Cleopatra | 2.77 | 2.82 | 2.77 |
| 20:00 | 1343 | Utsiktens BK vs Skovde Aik | 2.12 | 3.38 | 3.43 |
| 20:00 | 1558 | Orebro Syrianska vs Gefle IF | 3.07 | 3.61 | 2.01 |
| 20:00 | 2244 | Nosaby IF vs Eslovs BK | 2.15 | 3.50 | 2.87 |
| 20:00 | 2366 | Rosengard W vs Pitea W | 1.12 | 7.18 | 15.52 |
| 20:00 | 2943 | Umea IK W vs Kristianstads W | 4.19 | 3.65 | 1.70 |
| 20:00 | 3936 | BK Olympic vs Angelholms | 2.15 | 3.50 | 2.87 |
| 20:00 | 4384 | Sprint/Jeloy vs Start 2 | 1.58 | 4.76 | 3.88 |
| 20:00 | 4402 | Rosenborg BK 2 vs Tiller IL | 2.15 | 3.91 | 2.64 |
| 20:00 | 4893 | Akra vs FK Haugesund 2 | 1.52 | 4.76 | 4.27 |
| 20:00 | 5094 | Taby FK vs Vasalunds IF | 3.45 | 3.89 | 1.81 |
| 20:00 | 5384 | Yxhults IK vs Nordvarmland FF | 2.17 | 3.66 | 2.73 |
| 20:00 | 5442 | AS Douanes vs ASC Diambars | 2.91 | 2.57 | 2.72 |
| 21:00 | 1505 | Atletico Lanus W vs Racing Club | 5.61 | 5.03 | 1.38 |
| 21:00 | 5180 | CA Fenix vs CA Rentistas | 2.04 | 3.25 | 3.30 |
| 22:00 | 2238 | Al Ahly Cairo vs Wydad Casablanca | 3.01 | 2.86 | 2.39 |
| 22:00 | 3056 | Kansas City Nwsl vs Racing Louisville FC W | 2.45 | 2.94 | 2.84 |
| 22:15 | 5360 | Njarovik vs Reynir Sandgerdi | 1.35 | 5.26 | 5.84 |
| 23:30 | 2875 | SAO Paulo FC SP W vs Atletico Mineiro MG | 1.23 | 5.63 | 8.94 |
| 23:30 | 3723 | Sport Huancayo vs Alianza Atletico | 1.55 | 3.88 | 5.05 |

## JUMANNE - 31/05/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 00:00 | 4717 | Independiente Fbc vs Club Guarani De Trinidad | 2.20 | 2.83 | 3.41 |
| 00:00 | 5293 | 12 de Octubre de Itaugua vs Guairena FC | 2.77 | 2.97 | 2.48 |
| 01:00 | 4904 | Arnett Gardens FC vs Mount Pleasant FC | 4.77 | 3.79 | 1.60 |
| 01:00 | 5448 | Colo Colo vs Nublense | 1.60 | 3.71 | 4.88 |
| 02:00 | 1218 | Paysandu PA vs Manaus Fc/Am | 1.98 | 3.07 | 3.71 |
| 02:00 | 2065 | Anapolis GO vs Ceilandia Esporte Clube DF | 2.70 | 2.90 | 2.85 |
| 02:00 | 2183 | Internacional vs Atletico GO | 1.63 | 3.56 | 4.88 |
| 03:00 | 2292 | Alianza Lima vs Club Cienciano | 1.74 | 3.59 | 4.07 |
| 03:10 | 5487 | Deportivo Moron vs Deportivo Riestra | 2.10 | 2.72 | 3.89 |
| 20:00 | 2053 | Tegs SK vs Umeaa FC | 11.68 | 6.04 | 1.18 |
| 23:00 | 2071 | UTC Cajamarca vs Escuela Municipal Deportivo Binacional | 2.04 | 3.41 | 3.17 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# MO ATAKA MAAMUZI MAGUMU SIMBA SC

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Ahmed Ally, akiwapa pole wanachama na mashabiki wao kutokana na kipigo cha bao 1-0 walichokipata kutoka kwa watani zao wa jadi, Yanga kwenye mechi ya nusu fainali ya Kombe la FA, Mwenyekiti wa Heshima na Mwekezaji wa miamba hiyo, Dk. Mohamed "Mo" Dewji, ameitaka Bodi ya Klabu hiyo kufanya maamuzi magumu kwa manufaa na maslahi ya klabu hiyo.

**Baada ya kumalizika kwa mechi hiyo katika Uwanja wa CCM Kirumba juzi, Mo aliandika kwenye mtandao wake wa kijamii kuonyesha kuguswa na matokeo ya timu hiyo, lakini pia akiwapongeza watani wao wa jadi.**



Mwenyekiti na Mwekezaji wa Simba, Dk. Mohamed Dewj. **PICHA: MAKTABA**

Mbali na hilo, Mo amesema kuna haja ya kuangalia upya kikosi hicho na mipango kwenye bodi, akiongeza kuwa wachezaji wamekosa motisha, na njaa ya kushinda mataji msimu huu.

Kwenye ujumbe wake huo elekezi aliandika maneno haya.

"Hongereni watani, msimu huu umekua mbaya sana kwa Simba ukilinganisha na misimu mitano iliyopita, Bodi ya Simba inabidi ifanye maamuzi magumu kwa ajili ya msimu ujao, tunapaswa kuangalia upya timu na mipango kwenye bodi. Tunahitaji kujenga vizuri timu yetu na kuweka mikakati ambayo itaturudisha kwenye malengo yetu, timu imekosa motisha, na njaa ya kushinda mataji. Tumepungukiwa hamasa, ari ya kupambania mataji msimu huu." Aliandika.

Naye Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, amesema kuwa anafahamu namna ambavyo wanachama na mashabiki wa timu hiyo wanavyoteseka kutokana na matokeo mabovu msimu huu, lakini akawaahidi kuwa watafanya usajibu mkubwa kwa ajili ya msimu ujao.

"Niwape pole wanachama na mashabiki wetu, nafahamu namna ambavyo wanatesema na kuumia, ninajua machungu wanayopitia. Tumepoteza mchezo uliotegemea kurudisha furaha yetu msimu huu, lakini ungetufanikisha kufikia nusu ya malengo yetu msimu huu, lakini tumepoteza, ni majonzi makubwa, tumeumia, sisi kama utawala na wachezaji.

"Tulifanya kila njia kutwa mataji msimu huu, lakini mambo hayakuwa hivyo. Msimu huu sasa rasmi tumeumaliza, hatuna dalili yoyote ya kutwaa ubingwa, ndivyo mpira ulivyo, niwaahidi tu kuwa tumeona panapovuja, tunakwenda kufanya usajili babu kubwa ili msimu ujao tuwe imara zaidi," alisema kwa masikitiko.

Simba imetwaa Kombe la Mapinduzi pekee msimu huu ikilitema Kombe la FA, huku pia ikiwa na dalili zote za kukosa ubingwa wa Tanzania Bara iliyouhodhi kwa misimu minne mfululizo.

# *Mabondia wa Madola Tanzania wachapwa*

**Na Saada Akida**

MASHINDANO ya kimataifa ya ngumi za wazi ya ridhaa, yanayoendelea katika Uwanja wa Ndani wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, yameanza kwa kasi huku mabondia wa Tanzania wakianza kwa kuchezea kichapo.

Michuano hiyo imeandaliwa na Baraza la Michezo la Taifa (BMT) kwa kushirikiana na Shirikisho la Ngumi za Wazi Tanzania (OBFT), ikiwa na lengo la kuisaidia Tanzania kujiandaa na mashindano ya Jumuiya ya Madola yanayotarajiwa kutimua vumbi Julai 28 hadi Agosti 8, mwaka huu nchini Uingereza.

Pambano la kwanza kwa bondia wa timu ya Taifa ya Tanzania, Alex Isendi, lilianza kwa kukubali kichapo kwa pointi kwa majaji watatu kwa mmoja dhidi ya mpinzani wake kutoka Uganda, Tukamuhewe Joshua katika uzito wa Kg. 63.5.

Katika uzito huo Bondia wa Uganda, Senyange Zebra, alishinda kwa majaji wote watatu dhidi ya mpinzani wake kutoka Burundi, Nduwarugira Nestroy. Bondia wa Uganda, Kibira Owen aliibuka mshindi kwa kumtwanga kwa KO mpinzani wake kutoka Klabu ya Magereza ya Tanzania, Shaban Hamadi kwa uzito wa Kg. 67.

Katika uzito wa Kg. 75, bondia kutoka Uganda, Nkobeza Yussuph, ameshinda kwa RSCH (mpinzani kuokolewa na mwamuzi) dhidi ya Marko Francis wa Klabu ya JKT Tanzania.

Pambano hilo la mabondia wote kutoka Tanzania la uzito wa Kg. 52, Chinyemba Patrick, ameshinda kwa pointi kwa majaji wote watatu dhidi ya Yohana Kenneth wa JKT.

Uzito wa Kg. 48, Rahma Joseph wa JKT, ameshinda kwa pointi kwa majaji wote watatu kwa kumchapa kwa pointi Aisha Idd wa JKT.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkurugenzi wa Mashindano wa Maendeleo ya Michezo wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo Yusuph Singo, alisema kuandaa mashindano hayo ni jambo jema na bora kwa ajili ya maandalizi ya mabondia wetu kujiandaa na michezo ya Jumuiya ya Madola.

Kwa upande wa Katibu Mkuu Msaidizi wa OBFT, Mohamed Abubakar, ameishukuru serikali, kwa kuwezesha wanamichezo wanaojiandaa na michezo hiyo wakiwamo mabondia kukaa kambini tangu Februari mwaka huu na kuhakikisha maandalizi ya mashindano ya kimataifa ya majaribio yanafanyika kwa kuwawezesha kwa asilimia 100.

Michezo
Jumatatu Mei 30, 2022
Nipashe



Mo ataka maamuzi magumu Simba UKURASA 23



Wachezaji wa Real Madrid ya Hispania, viongozi na benchi la ufundi wakishangilia baada ya kukabidhiwa Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa kuifunga Liverpool ya England bao 1-0 kwenye mechi ya fainali iliyopigwa Uwanja wa Stade de France, Paris nchini Ufaransa juzi. **HABARI UK. 12+13. PICHA: MTANDAO**

# FEI TOTO AANIKA UDHAIFU SIMBA

**Adam Fungamwangwo na Shufaa Lyimo**

## Ataja kinachowatesa viungo, kocha Nabi naye afunguka mbinu...

KIUNGO wa Yanga, Feisal Salum 'Fei Toto', aliyefunga bao pekee kwenye mechi ya nusu fainali ya Kombe la FA dhidi ya watani wao wa jadi, Simba, amefichua siri kuwa baadhi ya wachezaji wa wapinzani wao hao wanaocheza eneo la kiungo wana tatizo la kasi.

**Fei Toto aliyefunga bao hilo dakika ya 25 ya mchezo kwa shuti kali la mbali, amesema aliwafanyia mazoezi ya siku tatu viungo wa Simba, baada ya kugundua kuwa hawana kasi.**

Mchezaji huyo anayesifika kwa mashuti ya mbali, alisema kuwa hawakuwa na muda mrefu wa kujiandaa na mechi hiyo, lakini walitumia siku tatu kuisoma Simba, ndipo alipogundua udhaifu huo.

"Nilikuwa nawaangalia viungo wa Simba wanavyocheza, uzuri wao na udhaifu wao, kuna baadhi ya wachezaji wanaocheza eneo la kiungo hawana kasi, ni wachezaji wazuri, lakini wana udhaifu huo, hivyo nikatafuta ni jinsi gani ya kuutumia udhaifu huo. Siyo kila mchezaji amekamilika, hata mimi nina madhaifu yangu," alisema Fei Toto ambaye pia huichezea Taifa Stars na timu ya Taifa ya Zanzibar, Zanzibar Heroes.

Alisema siri ya kupiga mashuti ni mazoezi binafsi ambayo anayafanya, lakini pia uthubutu kwani siyo kila shambulizi ni lazima wachezaji wafike hadi kwa golikipa.

"Nimefunga mabao haya msimu huu kama matatu hivi, unajua kuna maeneo ukisogea unaona umjaribu kipa, golikipa naye ni binadamu, zingine zinakataa, zingine huwa zinakubali. Nilisogea nikaona sikabwi, na kuna nafasi ya kupiga, nikapiga mwanangu kambani, mnyama kafa." Alisema huku akiangua kicheko.

Mchezaji huyo alijiunga na Yanga mwaka 2018 kwa namna ya kushangaza, kwani asubuhi alitambulishwa kama mchezaji wa Singida United, lakini jioni akatangazwa kuwa mchezaji wa Yanga. Kabla ya 'sinema' hiyo, mchezaji huyo alikuwa akiichezea JKU ya Zanzibar.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Klabu ya Yanga, Nasreddine Nabi, amesema walicheza vizuri zaidi ya wapinzani wao, Simba ndio maana wakafanikiwa kuwatoa kwenye michuano hiyo Kombe la Shirikisho la Azam (ASFC).

Akizungumza na gazeti hili Kocha huyo alisema: " Simba walicheza vizuri kipindi cha pili ni kawaida yao kupata magoli kipindi cha pili, lakini hata sisi tulipata nafasi nyingi za wazi hatukuongeza goli," alisema Nabi.

Alisema mchezo huo ulikuwa na ushindani na kudai anashukuru dakika 45 za kipindi cha kwanza timu yake iliweza kupata bao la kuongoza lililodumu hadi mwisho.

Kuhusu kucheza bila winga kwa kipindi kirefu cha mchezo, Nabi alisema aliamua kufanya hivyo baada ya kukosekana kwa wachezaji wake, Saido Ntibazonkiza na Dickson Ambundo ambao aliwasimamisha kwa utovu wa nidhamu.

Yanga sasa itakutana na Coastal Union katika mechi ya fainali itakayopigwa Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha Julai 2, mwaka huu. Coastal imeitoa Azam jana kwa penalti 6-5 katika nusu fainali ya pili iliyopigwa uwanjani hapo.

# Coastal yaifuata Yanga fainali FA

**Na Adam Fungamwango**

COSTAL Union ya Tanga ndiyo itakayocheza fainali ya Kombe la FA dhidi ya Yanga kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, jijini Arusha Julai 2, mwaka huu baada ya jana kuibwaga Azam FC kwa mikwaju ya penalti 6-5, baada ya dakika 120 zilizokuwa hazina bao lolote.

Penalti za Coastal ziliwekwa nyavuni na Muhsin Makame, Amani Kiata, Pascal Kitenge, Abdul Selemani 'Sopu', William Kisingi na Hamza Mubarak, huku Miraji Hassan akikosa.

Azam ambayo msimu uliopita ilitolewa pia kwenye hatua ya nusu fainali dhidi ya Simba kwa bao 1-0, penalti zake ziliwekwa wavuni na Rodgers Kola, Bruce Kangwa, Never Tegere, Aggrey Morris na Idriss Mbombo, Lusajo Mwaikenda aliyekosa penalti ya kwanza na Charles Zulu aliyeikosa ya mwisho. Hadi penalti tano-tano zinakamilika, timu zote zilikuwa zimeweka penalti nne kimiani na kukosa moja moja ndipo zilipofuata zile za piga nikupige kabla ya Azam kutolewa.

Ni mechi iliyokuwa na kosa kosa nyingi kwa pande zote mbili, lakini makipa wa pande zote Wilbroad Maseke wa Azam na Mohamed Hussein wa Coastal Union wakikaa imara kuokoa michomo mikali.

Kama Coastal ingekuwa makini ingeweza kupata ushindi ndani ya dakika 30 za nyongeza, kwani Azam FC walionekana kuchoka na 'Wagosi wa Kaya' walifanya mashambulizi mengi kipindi hicho, lakini mabeki wa timu hiyo wakiongozwa na Morris, Kangwa walikaa imara kuokoa hatari.

Kwenye mechi ya robo fainali, Coastal Union pia iliitoa Kagera Sugar kwa mikwaju ya penalti 5-4, baada ya kutoka sare kwa dakika 90 za mchezo. Kwa matokeo hayo, sasa fainali ya kombe hilo Yanga itacheza dhidi ya Coastal na mshindi atakayetwaa ubingwa atakwenda kuiwakilisha Tanzania kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Hata hivyo, ni Coastal ndiyo itakuwa inatafuta tiketi hiyo, kwani Yanga tayari ina tiketi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika, kwani iko kwenye timu mbili za juu kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042